


UKURASA 3



**CCM** yabaini tatizo kwa wanachama wenye nguvu




UKURASA 9


# Nipashe JUMAPILI

MWANGA WA JAMII

Jumapili Oktoba 23, 2022 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • No. 0581107


www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper LIKE & FOLLOW US


RIPOTI MAALUM

# Siri wanaume kufa mapema

**MADAKTARI** bingwa, wanasaikolojia wafichua yaliyojificha... *Endelea ukurasa 4 na 5*




**MAGONJWA**

1. OTHER SEPSIS
2. CARDIOMYOPATHY
3. HEART FAILURE
4. HIV & TB
5. HIV/AIDS
6. HYPERTENSIVE HEART DISEASE
7. PNEUMONIA
8. KIDNEY FAILURE
9. HAEMORRHAGE
10. AMOEBIASIS

Vifo vilivyorekodiwa katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Shinyanga mwaka 2021.
**CHANZO:** Ofisi ya Mratibu wa Takwimu za Afya Mkoa wa Shinyanga. Septemba 29, 2022.

WANAUME WANAWAKE

# Moto waibuka tena Mlima Kilimanjaro

UKURASA 2




# CHADEMA yakosoa ripoti ya Kikosi Kazi



UKURASA 2

MICHEZO SIMBA SC, YANGA HESABU UWANJANI UK. 24 MAONI, KATUNI UK.6



Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye (kulia), akipata maelezo kutoka kwa mmoja wa wanafunzi waliopata mafunzo katika Taasisi ya Apps & Girls inayofadhiliwa na Tigo, Maria Mtega (katikati), kuhusu jinsi roboti maalumu inavyofanya kazi katika kukabiliana na ongezeko la hewa ya ukaa, jijini Dar es Salaam jana. Wanafunzi hao, walishiriki mashindano ya ubunifu katika sekta ya Teknolojia Habari na Mawasiliano (TEHAMA), yaliyomalizika hivi karibuni nchini Uswisi ambapo Tanzania ilishika nafasi ya pili. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Moto waibuka tena Mlima Kilimanjaro

**Na Godfrey Mushi,**
MOSHI

MOTO ambao chanzo chake hakijajulikana umezuka ndani ya Hifadhi ya Taifa Kilimanjaro (KINAPA), eneo la kupumzikia wageni maarufu Karanga Camp, kuelekea Baranco na kuteketeza sehemu kubwa ya miti ya asili ya hifadhi hiyo.

Tukio la moto kama huo lilitokea Oktoba 11, 2020 katika eneo la Whona, ambacho ni kituo cha kupumzikia wageni wanaotumia njia ya Mandara na Horombo.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA) kupitia kwa Ofisa Uhifadhi Mwandamizi (Mawasiliano), Catherine Mbena, moto huo uligunduliwa usiku wa Oktoba 21 mwaka huu katika Kituo cha Karanga.

"Hatua za haraka ambazo tumechukua ni kwamba, tayari askari wa TANAPA wakishirikiana na Jeshi la Zimamoto na Ukoaji, Polisi, Mgambo, wanafunzi wa Chuo cha Kimataifa cha Usimamizi na Uhifadhi wa Wanyamapori-Mweka na wafanyakazi wa kampuni inayoendesha shughuli za utalii ya ZARA Tours, wako eneo la tukio kuudhibiti moto huo,"alisema Mbena.

Taarifa zinadai kuwa moto huo ulisambaa kwa kasi zaidi ulipofika eneo la ukanda wa Moorland, ambako mimea yake ikishika moto huwa mkali.

Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu alisema hadi jana mchana, moto huo ulikuwa haujasababisha madhara yoyote kwa watalii na jitihada za kuudhibiti zilikuwa zinafanywa na askari zaidi ya 350 waliopelekwa katika hifadhi hiyo kuudhibiti moto huo uliozuka katika kituo hicho kilichoko mita 3,963 kutoka usawa wa bahari.

Kamishina wa Uhifadhi wa Kanda ya Kaskazini, Betrita James alisema baada ya kupata taarifa za kuonekana kwa moto huo, menejimenti ya Hifadhi ya Taifa Kilimanjaro ilikusanya nguvu kazi, vifaa na timu ya watu mbalimbali na wadau wengine kwa ajili ya kusaidia juhudi za kuuzima.

Kaimu Mkuu wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Mkoa wa Kilimanjaro, Abraham Ntezidyo alisema jitihada za kuuzima moto huo zinaendelea mlimani na baada ya kutoka eneo la tukio watafanya tathmini.

Kanzidata ya Hifadhi ya Taifa Kilimanjaro inaonyesha kuwa mwaka 2015/16 eneo lililoteketea kwa moto ni hekta 49.13, mwaka 2016/17 hekta 17, mwaka 2017/18 hekta 82, mwaka 2018/19 hekta 72.3, mwaka 2020 hekta 22.05.

Kwa kipindi kisichozidi miaka mitano hadi kufikia mwaka 2020, jumla ya hekta ambazo ziliteketea kwa moto katika hifadhi hiyo zinatajwa kufikia 242.48, huku sababu kubwa ya kuzuka kwa moto katika eneo hilo ikielezwa ni uvunaji mbaya wa asali, ujangili na njia mbaya za kilimo.

**JICHO LA CAG**

Katika ripoti yake ya ukaguzi kwa mwaka 2020/21 iliyotolewa Machi 30, mwaka huu, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) amefanya uchunguzi kuhusu ripoti ya tukio la moto KINAPA iliyotolewa Desemba 2020 na kutoa mapendekezo manne kwa mamlaka husika.

CAG Charles Kichere, mbali na mambo mengine, anasema moto huo ulisababisha hasara ya jumla ya Sh. bilioni 1.214 na kubainisha kuwa mamlaka za hifadhi za taifa hazina uwezo wa vifaa na maandalizi kupambana na majanga ya asili.

## CHADEMA yakosoa ripoti ya Kikosi Kazi

**Na Romana Mallya**

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kimeibuka na kukosoa ripoti ya Kikosi Kazi cha kuratibu maoni ya wadau wa demokrasia na vyama vya siasa huku kikitaka serikali iruhusu mikutano ya hadhara.

Hatua hiyo imekuja ikiwa ni siku moja baada ya kikosi kazi kukabidhi ripoti yenye mapendekezo 18 kwa Rais Samia Suluhu Hassan.

Akizungumza jana mkoani Dar es Salaam, Katibu Mkuu wa chama hicho, John Mnyika, alisema katika uchambuzi wao wa awali kuhusu mikutano ya hadhara ya vyama vya siasa, alisema jambo hilo lilitakiwa kutolewa uamuzi wa haraka.

"CHADEMA kinatoa wito kwa serikali kujitokeza bila kusubiri marekebisho ya Kanuni ya Vyama vya Siasa mwaka 2019, marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa, iondoe zuio walililoiita hili haramu la mikutano ya hadhara," alisema.

Mnyika alisema katika jambo hilo wanasisitiza kuwa azimio lililotolewa na Kamati Kuu ya CHADEMA Septemba 17 na 19 mwaka huu, pamoja na kutoa wito wa kuondoa zuio hilo, ilitoa maelekezo kwa ngazi zote za chama kuendelea na maandalizi ya mikutano ya hadhara katika tarehe ambayo itatangazwa.

"Chama kitaendelea kutimiza haki ya kikatiba na kisheria kufanya mikutano ya hadhara kwa mujibu wa kifungu cha 11 cha Sheria ya Vyama vya Siasa na vifungu vya 43 mpaka 46 vya Sheria ya Jeshi la Polisi," alisema.

Katibu Mkuu huyo alisema jambo hilo lilikuwa rahisi ambalo lilitakiwa kutolewa uamuzi kwa mujibu wa vifungu hivyo vya sheria.

Kuhusu mchakato wa katiba mpya, Mnyika alisema Mwenyekiti wa kikosi kazi alieleza kuwa walipokea maoni ya aina mbili, kundi lililosema hakuna sababu ya kuandikwa kwa katiba mpya ila kama kuna marekebisho yafanyike na la pili la maoni yaliyogawanyika makundi matano.

Alisema mwenyekiti aliligawa kundi la pili linalotaka katiba mpya katika makundi madogo matano, lakini hakutoa sababu za msingi za kuachana na kundi ambalo yeye alilitaja ni la tatu lililosema mchakato huo uendelee kwa kuondoa ulikokwamia kuanzia rasimu ya pili ya Tume ya Mabadiliko ya Katiba maarufu 'Tume ya Jaji Warioba'.

Alisema mwenyekiti hakutoa sababu za msingi, badala yake akarukia na kusema kikosi kazi kimekubaliana na maoni yanayosema, liundwe jopo la wataalam ambalo litaandaa rasimu ya tatu ya katiba na kupeleka bungeni kupitishwa kabla ya kupigiwa kura ya maoni.

"Hapa ndipo ilipo dhamira mbaya na nia ovu ya kikosi kazi. Bunge la sasa na umma unajua lilivyopatikana katika uporaji wa ridhaa ya wananchi ulioitwa Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020.

"Bunge hilo sasa ndo eti linakwenda kukabidhiwa kazi tukufu na kazi takatifu kupitia rasimu ya tatu ya katiba, Bunge la namna hii lenye hodhi ya chama kimoja likiruhusiwa kufanya kazi hii litakwenda kuharibu zaidi.

"Kitakachotoka kitakuwa kibaya kuliko rasimu ya Jaji Warioba au Katiba Pendekezwa, kitakuwa kibaya zaidi na sumu ya kuua mchakato wa katiba mpya au kuuvuruga kupindukia mchakato huo," alisema.

Mnyika alisema CHADEMA ilitarajia kikosi kazi kingekuja na mapendekezo ya ama kutengenezwe chombo cha kitaifa chenye kuundwa na wawakilishi wa wananchi kutoka makundi mbalimbali au wajumbe wa kuchaguliwa, kwa minajili ya kufanya kazi ya kutunga katiba mpya.

Alisema mapendekezo ya kikosi kazi hicho, yangekuwa na mantiki, kama yasingelihusisha Bunge katika kupitisha rasimu ya tatu ya katiba mpya.

Pia alisema hatua iliyofanywa ya pili ya kuhusisha Sheria ya Mabadiliko ya Katiba na Sheria ya Kura ya Maoni ilipaswa iwe hatua ya kwanza na ingepelekwa Bunge la mwezi Novemba ili kukwamua na kukamilisha mabadiliko ya katiba.

Pia alisema hatua iliyofanywa kwanza na kikosi kazi hicho ya mjadala wa kitaifa wa kupata muafaka katika masuala ya msingi, ingekuwa ndiyo hatua ya pili, kwa muswada wa sheria kupelekwa bungeni ili kuweka utaratibu wana namna gani ya kuendesha mjadala wa kitaifa vyombo vipi vitumike.

Mnyika alisema hatua waliyoitaja ni ya tatu ya kuundwa kwa jopo la wataalam, ingekuwa ni ya nne ambayo ingehusisha kuweka katika maandishi huo muafaka wa kitaifa kutafsiri kutoka katika lugha ya kisiasa, lugha ya kijamii na ya kiuchumi na kuwa lugha ya kisheria.

Alisema utaratibu uliopendekezwa na kikosi kazi ni mbovu usiokuwa na ratiba, utaratibu na muundo muafaka wa kujenga muafaka wa kitaifa.

Alisema CHADEMA itaendelea kulinda maoni ya wananchi kuhusu haja ya katiba mpya.

Kuhusu tume huru ya uchaguzi, chama hicho kilisema kuwa, walitarajia kingekuja na mapendekezo yaliyochambua Mkataba wa Afrika wa masuala ya demokrasia, utawala na uchaguzi ambao umeweka misingi, tume inapaswa iundwe vipi.

"Wangekuja na utafiti, na utafiti tayari Tume ya Jaji Warioba ilishaufanya, wangeurejea kitabu cha utafiti wangeangalia nchi nyingine zenye miundo bora ya tume ya uchaguzi, wangekuja na mapendekezo ambayo yeyote angeona angesema hii ni Tume Huru ya Uchaguzi.

Alisema ili waendelee na mchakato wa katiba ulipokwamia, rasimu ya Tume ya Mabadiliko ya Katiba ndipo pawe pa kuanzia.

Kuhusu pendekezo la sheria ya vyama vya siasa ifanyiwe marekebisho ili kulipatia baraza la vyama lililoundwa na vyama vyenyewe mamlaka ya kushughulia uvunjifu wa maadili ya vyama kupitia kamati ya maadili, Mnyika alisema lina dhamira ya kuthibiti vyama vikuu vya upinzani hasa CHADEMA.

Mnyika alisema CHADEMA kinaitaka serikali iweke wazi gharama ambazo kikosi kazi imezitumia.

HABARI KITAIFA

# Polisi wakoleza vita dhidi ya ukatili kijinsia

**Na Thobias Mwanakatwe,** IKUNGI

KATIKA kukabiliana na matukio ya ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto wilayani Ikungi mkoani Singida, uongozi wa Jeshi la Polisi umesema unachukua hatua kali dhidi ya watuhumiwa ambapo watu wawili wamehukumiwa vifungo miaka 30 jela na mmoja kifungo cha maisha ndani ya kipindi cha miezi miwili.

Mkuu wa Polisi Wilaya ya Ikungi, Suzana Kidiku alibainisha hayo jana wakati Shirika la Empower Society Transform Lives (ESTL) linalojihusisha na masuala ya kupinga ukatili wa kijinsia, lilipozindua rasmi huduma za elimu na uwezeshaji jamii kwenye wilaya hiyo.

Alisema Jeshi la Polisi limekuwa kwenye harakati mbalimbali za kukabiliana na matukio ya ukatili wa kijinsia kwa nyakati tofauti ambapo katika kipindi cha mwezi Julai hadi Septemba mwaka huu limefanikiwa kunusuru kwa kuwarejesha shuleni wanafunzi watatu ambao walikuwa hatarini kukatisha masomo yao kutokana na matukio ya ukatili.

Kidiku alisema jeshi hilo katika kipindi hicho limefanikiwa kufikisha kesi tatu za matukio ya ukatili wa kijinsia kwenye vyombo vya sheria ambapo mahakama iliwakuta watuhumiwa na hatia na wawili walihukumiwa vifungo vya hadi miaka 30 huku mmoja akiadhibiwa kifungo cha maisha.

Mkaguzi wa Uhamiaji Wilaya ya Ikungi, Abel Shindayi alisema kuna haja mamlaka za elimu kufanya marekebisho ya mfumo wa mtaala wa elimu uliopo kwa kuongeza kipengele cha somo la ukatili wa kijinsia ili wanafunzi wafundishwe na kuwa na uelewa mpana wa masuala hayo.

Mkurugenzi wa ESTL, Joshua Lisu alisema Wilaya ya Ikungi ina vihatarishi vikubwa vya matukio ya ukatili kwa wanawake na watoto kutokana na jiografia yake ya mipaka na wilaya za jamii ya wafugaji za Hanang (Manyara) na Kondoa (Dodoma) ambazo zimegubikwa na matukio ya ukeketaji.

Alisema shirika hilo lisilo la kiserikali kwa udhamini wa Ubalozi wa Finland, Uholanzi na Shirika la Foundation Civil Society (FCS) katika kipindi cha miaka minne (2018-2022 limefanikiwa kuzifikia takribani kata 28 ndani ya Wilaya za Singida Manispaa na Singida Vijijini kwa utekelezaji wa huduma kama hizo.

Huduma nyingine walizofanikiwa kuzitoa kwenye maeneo hayo ni pamoja na uanzishwaji wa utaratibu wa utoaji huduma mbalimbali ndani ya eneo moja (One Stop Centre), uundaji wa kamati za MTAKUWWA zipatazo 39 sambamba na uanzishaji wa mfumo maalum wa TEHAMA ambao umekuwa ukifanya kazi ya kufuatilia kesi za matukio ya ukatili.

# CCM yabaini tatizo kwa wanachama wenye nguvu

**Na Maulid Mmbaga**

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Changolo amesema moja ya shida zinazowakabili ni kuwapo baadhi ya wanachama ndani ya chama hicho wanaotengeneza alichokiita miundombinu haramu ya kuwadhibiti watu wazuri kupata nafasi.

Akizungumza jana alipozindua ofisi ya chama Wilaya ya Kigamboni na nyumba ya Katibu wa CCM Mkoa wa Dar es Salaam, Chongolo alisema chama hicho kina watu wazuri, bora na wenye nia njema, lakini tatizo kuna watu wanaotengeneza mazingira ya kuwakosesha dhamana. Kutokana na hilo, mtendaji huyo wa chama alitoa angalizo kwa watu hao kuacha mara moja vitendo hivyo huku akieleza kwamba kwa idadi ya mikoa 32 iliyopo ni michache na haitawanyima fursa ya kupitia jina moja baada ya lingine katika orodha ya walioomba kuchaguliwa.

"Tutapitia maelezo binafsi na mengine na tutajiridhisha kwa kila mtu ili tupate viongozi ambao wanafanana na mazingira na wana dhamira ya kweli ya kuendeleza utumishi na uhai wa chama chetu mbele na siyo bora viongozi, kwenye hilo wala nisiwadanganye hatutaacha kulifanya.

"Nisipoisema hivyo nitakuwa sitendi haki na hilo wala halihitaji makofi kwa sababu ni dhamira yenye lengo zuri kwa chama chetu. Pia tuna dhamana ya kusimamia utekelezaji wa ilani, tuna wajibu wa kutekeleza miradi ya maendeleo, kuisimamia na kuhakikisha inatekelezwa kwa kiwango chenye tija," alisisitiza Chongolo.

Alibainisha kuwa uchanguzi wa mwaka 2025 hawatachaguliwa kwa sababu wana sare nzuri ya chama, bali watachaguliwa kwa namna watakavyofanya kazi kwa kiwango chenye tija na kutatua shida za wananchi, huku akitoa wito kwa viongozi kulipa kipaumbele suala hilo.

Alisema kuwa kila mtu alichaguliwa kwa kuomba ridhaa mwenyewe na hakuna mtu aliyefuatwa nyumbani akachukue fomu ya kugombea, hivyo alisisitiza baada ya uchaguzi, wana wajibu nyuma na mbele yao wa kusimamia na kutekeleza ilani ya chama chao.

Pia alisema wana shida ya rushwa ndani ya chama hicho n kwamba katika ngazi ya wilaya, walibaini baadhi ya watu kufanya rafu na kukiuka taratibu kwenye uchaguzi, jambo lililosababisha kufutwa kwa uchaguzi kwenye wilaya 21 na kurudiwa upya.

"Kwenye ngazi ya mkoa macho yetu yako wazi, tunatazama mchakato kwa karibu na hatutasita kuchukua hatua popote tutakapoona kuna jambo lisilokuwa na heri kwenye chama chetu," alionya.



Nguzo ya nyaya za simu ikiwa imeinama na kusababisha usumbufu kwa magari na wapita njia katika eneo la Goba, barabara ya kuelekea Makongo Juu, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Tathmini uhaba chakula yaanza rasmi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAKALA wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA), umeanza kufanya tathmini ya kina kwenye maeneo yenye uhaba wa chakula ili yasaidiwe.

Aidha, umepeleka tani 3,000 za nafaka kwenye Halmashauri za Bunda, Sengerema, Geita, Nzega, Liwale, Nachingwea, Longido, Loliondo na Monduli ili kuuzwa kwa bei nafuu kutokana na maeneo hayo kukabiliwa na mfumuko wa bei.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa NFRA, Milton Lupa, aliyasema hayo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa kuhusu vipaumbele vya mwaka 2022/23.

Alisema tathmini hiyo hadi sasa inafanyika kwenye halmashauri nane ambazo zimewasilisha maombi yao.

Ofisa mtendaji mkuu huyo alisema NFRA iko tayari kuhudumia maeneo yatakayothibitika kuwa na upungufu wa chakula ili kuleta unafuu kwa wananchi.

"Nchi ina utoshelevu wa chakula baada ya kupata tathmini ya kina kuhusu maeneo halisi ambayo yameathirika, kuna timu kwa sasa inafanya tathmini ya kina, tathmini ya awali ilishafanyika na itakapotoka sisi kama wakala tumejipanga kuhakikisha maeneo hayo tunatatua upungufu wa chakula," alisema.

Alisema kuwa tathmini hiyo inafanywa na Ofisi ya Waziri Mkuu Idara ya Maafa, Wizara ya Kilimo na halmashauri husika.

"Timu iliketa mapendekezo yao huwa tunaelekeza kupeleka chakula maeneo hayo na bei inategemea maeneo yenyewe, kuna baadhi ya maeneo watu hawana uwezo wa kununua chakula kamati ile huwa inaleta mapendekezo, mengine huwa mkauze kwa bei nafuu na tukikuta wananchi wanashindwa hata kununua kwa bei nafuu basi Wizara ya Kilimo wanaleta mapendekezo kuwa kama maeneo yana hali hiyo kiuzwe kwa bei hii,"alisema.

Alihimiza wananchi kuhakikisha wanahifadhi akiba ya kutosha ya chakula kipindi cha mavuno na kuuza chakula pale wanapokuwa na ziada katika uzalishaji.

"Wakiuza chakula chote ni tatizo kwa kuwa nchi zinazotuzunguka wengi wana changamoto ya chakula. Wakala umejipanga kuendelea kuwa na akiba ya kutosha maana Desemba hadi Machi huwa hali ni mbaya hasa kwa wananchi wenye kipato cha chini," alisema.

Awali, alisema ununuzi wa akiba ya chakula umeongezeka kutoka tani 58,000 hadi 110,000 huku msimu mwaka 2022/23, unaendelea kwenye mikoa mbalimbali.

"Lengo kupitia mradi wa vihenge na maghala ni kuongeza uwezo wa kuhifadhi kutoka tani 251,000 hadi 501,000, upo kwenye hatua mbalimbali za utekelezaji," alisema.


**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

**MEDARD RWEYEMAMU METHODIUS** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 420 CVG – TOYOTA IST.** Chassis namba **NCP600203619.** Engine namba **2N23502039.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **ARU/ARU/RB/413634/2022.**

**FOMU YA MIRATHI-2**
**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA MWANZO**
**WILAYA YA MOROGORO**
**MKOA MOROGORO**
**KITUO CHA MJINI**
**Usimamizi wa Mirathi Na. 65/2022**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHENU ABDALLAH YUSUPH SARANJE WA KICHANGANI KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOTOLEWA NA RAJABU ABDALLAH SALANJE MAHAKAMANI /GAZETI**

**TANGAZO**

(Kanunu ya 5 (2) kanuni za usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 24/ Mwezi 10 Mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Zingatia;

Endapo kuna yeyeto mwenye Wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.

* Wosia wa Marehemu huyu upo Mahakamani na waweza kukaguliwa
* Marehemu hakuacha wosia
* Futa isiyohusika

**Imetolewa leo tarehe 20 mwezi 9 mwaka 2022**



RIPOTI MAALUM

# Siri wanaume kufa mapema

## •Madaktari bingwa, wanasaikolojia wafichua yaliyo nyuma ya pazia

**Na Sanula Athanas,**
aliyekuwa SHINYANGA

NI majira ya jioni, jua likiashiria machweo yanakaribia katika Kitongoji cha Bukengwa, Kijiji cha Masunula, Kata ya Usule, Wilaya ya Shinyanga mkoani Shinyanga. Kwa mbali anaonekana babu akikata kipande cha gazeti ili kutengeneza sigara yake ya kienyeji.

Mahali hapo ni umbali wa Km 33.5 kusini magharibi mwa Mji wa Shinyanga na safari yake kwa gari kutoka mjini inachukua takriban saa moja kutokana na mzunguko mrefu wa kuifuata barabara kuu ya lami ya Shinyanga-Kahama kisha unapofika Kijiji cha Ishinabulandi (12.8 kutoka mjini) unachepuka kulia kuifuata barabara ya vumbi ukipitia vijiji jirani vya Igegu, Mwamala, Bunonga na Sumbigu.

Akiwa ameketi kwenye kigoda, nje ya nyumba yake iliyojengwa kwa ukuta wa udongo, juu imeezekwa kwa bati, Mzee Matongo Machalilo, ambaye wajihi wake unaonesha amekula chumvi nyingi, anasikiliza wimbo unaoitwa 'Yamumakaya' (mambo ya ndani ya kaya) uliotungwa na msanii wa nyimbo za asili, Bahati Bugalama (pichani)

Kila unapofika mwisho wimbo huo ulioimbwa kwa lugha ya Kisukuma, mzee huyo anaurudia kupitia redio yake ndogo ya kisasa inayotumia nishati ya jua huku akionesha umakini mkubwa katika kufuatilia kinachoimbwa.

Hapo ndipo Nipashe inapoguswa na kinachojiri na kuamua kusogea kwa Mzee Machalilo ili kupata tafsiri na ujumbe uliokusudiwa na mtunzi wa wimbo huo.

Babu huyo mwenye umri wa miaka 86 anasema ujumbe uliomo ndani ya wimbo huo uliogusa hisia zake, ni swali linalohitaji majibu 'kwanini wanaume wanakufa mapema zaidi kuliko wanawake?'

"Mjukuu wangu (mwandishi wa Nipashe) huyu msanii anasema katika kaya ambazo zimepoteza mzazi mmoja, zinaonyesha wanaume wanakufa kwa wingi na kuwaacha wake zao wakiwa wajane.

"Hata nikiangalia hapa kwenye kitongoji chetu (Bukengwa), anachokiimba Bugalama kina uhalisia. Tuna kaya nyingi zenye wajane kuliko wagane. "Ninafikiri ninyi wasomi mnapaswa kumjibu huyu msanii -- kwanini sisi wanaume tufe mapema zaidi kuliko wanawake?" Mzee Machalilo anawasilisha hoja hiyo kwa Nipashe.



Katika udadisi wake, Nipashe inabaini kwamba hiyo ni familia ya pili kwa Mzee Machalilo, akimrithi mke wa kaka yake aliyefariki dunia miongo mitatu iliyopita na ana familia nyingine iliyoko kitongoji jirani kijijini huko.

Vilevile, katika kufanyia kazi hoja ya babu huyo kuhusu uwiano wa wagane na wajane kijijini Masunula, Nipashe ilizungumza na Mwenyekiti wa Kitongoji cha Bukengwa, Kajala Kajigo aliyebainisha kuwa hadi siku hiyo (Septemba 27, mwaka huu), Kitongoji cha Bukengwa kilikuwa na jumla ya kaya 54.

Kwa mujibu wa Kajigo, kati ya kaya hizo, 10 zina wajane huku nne (4) zikiwa na wagane, takwimu zinazoakisi ujumbe uliotawala katika wimbo wa 'Yamumakaya' wa msanii Bugalama.

Nipashe pia ilizungumza na Mwenyekiti wa Kijiji cha Masunula, Ilimba Magohe ambaye alisema uzoefu wake wa miaka saba kukiongoza kijiji hicho unaonesha kuna idadi kubwa ya vifo vya wanaume kijijini humo kulinganishwa na wanawake ingawa hakuwa na takwimu halisi za kuthibitisha kauli yake.

### VIFO SHINYANGA

Katika kusaka majibu ya hoja ya msanii Bugalama, Nipashe inatua mezani kwa Mratibu wa Takwimu za Afya Mkoa wa Shinyanga, Allan Luvanda anayebainisha kuwa kwa mwaka 2021, Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Shinyanga ilikuwa na vifo vya wagonjwa 1,518.

Luvanda anafafanua kuwa, kati ya vifo hivyo, 953 ni vya wanaume (asilimia 62.78) na vifo 565 vya wanawake (asilimia 37.22). Takwimu hizo zina maana kwamba vifo vya wagonjwa wanaume ni takriban theluthi mbili ya vifo vyote hospitalini hapo.

Nipashe pia inabaini kwamba magonjwa ya kifua kikuu (TB) na Ukimwi yanaongoza kwa kusababisha vifo vingi katika hospitali hiyo, yakiwa na jumla ya vifo 516 (asilimia 33.99 ya vifo vyote). Kati yake, vifo vya wanaume ni 345 (asilimia 66.86).

Kwanini wanaume waongoze kwa vifo vya Ukimwi? Mratibu wa Kudhibiti Ukimwi Mkoa wa Manyara, Dk. Charles Shija, ana ufafanuzi katika hilo, akitamka:

"Wanaume sio wepesi wa kupima afya zao, wanawake wananufaika katika hilo maana si tu kwamba ni wepesi wa kutaka kujua hali zao kiafya, bali pia wanapofika hospitalini au kituo cha afya kuanza kliniki ya ujauzito, wanapimwa kujua hali ya maambukizo ya VVU (Virusi vya Ukimwi).


"Kwa hiyo, wanawake wengi hugundulika kuwa na VVU kabla ya kufikia kwenye hatua ya Ukimwi wakati wanaume wengi hugundulika kipindi ambacho virusi vimeingia katika hatua ya Ukimwi. Ndio maana wanawake wanaongoza kwa maambukizo ya VVU lakini wanaume wanaongoza kwa vifo vya Ukimwi."

Ni hoja inayoungwa mkono na Nyangusi Laiser, Ofisa Ufuatiliaji na Tathmini wa Tume ya Taifa ya Kudhibiti Ukimwi (TACAIDS), anayebainisha kwamba mwaka 2020, Tanzania ilikuwa na maambukizo mapya ya VVU kwa watu 68,000. Kati yao, 37,000 ni wanawake (asilimia 54.4) na wanaume 21,000.

### TAKWIMU ZA VIFO HOSPITALINI

VIFO 2021

| S/N | Chanzo cha kifo | Wanaume | Wanawake |
|---|---|---|---|
| 1 | Other sepsis | 112 | 44 |
| 2 | Cardiomyopathy | 98 | 16 |
| 3 | Heart failure | 51 | 66 |
| 4 | HIV & TB | 234 | 70 |
| 5 | HIV | 111 | 101 |
| 6 | Hypertensive heart diseases | 45 | 14 |
| 7 | Pneumonia | 67 | 25 |
| 8 | Chronic kidney disease [chronic renal failure] | 78 | 69 |
| 9 | Haemorrhage | 87 | 109 |
| 10 | Amoebiasis | 70 | 51 |




Vifo vilirekodiwa katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Shinyanga mwaka 2021. **CHANZO: Ofisi ya Mratibu wa Takwimu za Afya Mkoa wa Shinyanga, Septemba 29, 2022.**

Vilevile, Meneja wa Mfuko wa Udhamini wa Kudhibiti Ukimwi Tanzania (ATF), Peter Kivugo, akichangia hoja hiyo, anasema: "Vifo vinavyotokana na magonjwa nyemelezi kwa wanawake vimepungua lakini kwa wanaume vinapanda, wengi wanakufa mapema kutokana na kushindwa kuzingatia maelekezo ya dawa na kujizuia katika tabia hatarishi ambazo zinawasababisha kupata maambukizo mapya na magonjwa mengine ya zinaa."

Kivugo anarejea takwimu za vifo vitokanavyo na Ukimwi kwa mwaka 2019, akibainisha vilikuwa 21,529 kwa watu wenye umri wa kuanzia miaka 15, wanaume wakiwa 12,225 (asilimia 56.8) na wanawake 9,304 huku watoto chini ya miaka 15 vilikuwa 5,900 na kufanya jumla ya vifo 27,429.

### KULIKONI WANAUME?

Ikirejewa hoja ya msanii Bugalama, Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Moyo katika Hospitali ya Rufani ya Kanda Mbeya, Dk. Isakwisa Mwakyula anasema vipo vyanzo vingi vinavyosababisha wanaume kufa mapema zaidi kuliko wanawake, baadhi ya sababu ni za asili.

Anasema moja ya sababu hizo ni tofauti ya wingi wa homoni kinga (vichochezi) vya mwili ambavyo kitaalamu vinaitwa 'Estrogen', akifafanua kuwa wanawake wanazo nyingi zaidi kuliko wanaume, hali inayowafanya wanaume kuwa katika hatari ya kufa mapema zaidi.

Dk. Mwakyula pia anasema wanaume wanakufa mapema kutokana na kufanya baadhi ya shughuli ambazo zinahatarisha maisha yao kuliko wanawake, ikiwamo kufanya kazi kwenye migodi, mitambo ya umeme na hata kushiriki vita na operesheni za kijeshi.

"Wanaume pia wana tabia ambazo zinawaweka katika hatari za kufa haraka kuliko wanawake kutokana na kunywa pombe kupita kiasi pamoja na kuvuta sigara ambazo hudhoofisha afya zao.

"Vilevile, wanaume wanakufa zaidi kwenye ajali kutokana na kutochukua tahadhari kama ilivyo kwa wanawake. Wanaume wanaoongoza kuendesha magari kwa mwendokasi kulinganishwa na wanawake.

"Wanawake huwa wanajihami zaidi wanapougua kwa kuwahi kupata matibabu kuliko wanaume, hali ambayo husababisha wanaume kufa mapema kwa sababu huwa wanakwenda hospitalini wakiwa na hali mbaya.

"Ukienda katika hospitali yoyote, idadi ya wanawake waliolazwa huwa ni kubwa kuliko idadi ya wanaume, lakini pia wanaume hao unakuta wana hali mbaya kuliko inavyokuwa kwa wanawake.

"Wanawake ni wepesi wa kufunguka na kueleza kwa watu, hasa wanawake wenzao matatizo yanayowapata, hivyo hufarijiana, jambo ambalo ni gumu kwa wanaume," anafafanua.

Ili kukabiliana na tatizo hilo la wanaume kufa mapema kuliko wanawake, Dk. Mwakyula anashauri wanaume kubadili tabia kwa na kujijengea utaratibu wa kuwahi hospitalini kupata matibabu wanapojisikia kuugua, hivyo kupata matibabu mapema na kuepuka vifo.

Pia anawataka wanaume kuacha kunywa pombe kupita kiasi na kuvuta sigara kwa kuwa matumizi ya vileo hivyo ni hatari kwa afya zao na yanachangia vifo vya mapema.

"Kuhusu suala la utofauti wa vichocheo vya mwili, hili ni suala la asili ambalo hatuwezi kukabiliana kwa namna yoyote. Haya mengine inawezekana kabisa kukabiliana nayo. Hivyo, wanaume lazima wabadili tabia," Dk. Mwakyula anahitimisha.

INAENDALEA UK. 5

RIPOTI MAALUM

# Siri wanaume kufa mapema

INATOKA UK. 4

Kamishna wa Mamlaka ya Kuzuia na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA), Gerald Kusaya, anaungana na Dk. Mwakyula kutoa hadhari dhidi ya matumizi ya vileo, hasa dawa za kulevya, akionya kuwa mbali na kusababisha vifo, pia ni chanzo cha kuvurugika kwa afya ya akili, saratani ya viungo vya mwili kama mapafu, maini na moyo.

**MSAIKOLOJIA ANENA**

Msaikolojia Tiba, Geofrey Mwamnyanyi anayefanya kazi na shirika la lisilo la kiserikali la Initiative of Change, anasema wanaume wanawahi kufa kutokana na sababu za mfumo wa mwili na za kisaikolojia.

"Asili ya kuumbika kwao inafungwa kwenye seli za mwili ambazo hazina uhai wa muda mrefu. Kama mwanamke na mwanamume wanatengenezwa kwenye mazingira ya aina moja, basi mwanamke ana uwezo wa kuishi miaka mitano zaidi, kama mwanamke anaishi miaka 80, mwanaume ataishi miaka 75," anasema.

Mwamnyanyi anasema sababu za kisaikolojia zinaathiri mfumo wa maumbile, akifafanua kuwa wanaume wameumbwa wakiwa na nguvu ya kufanya uamuzi wakati mifumo ya kimaumbile inafanya wanawake wawe na nguvu zaidi kihisia kuliko wanaume.

"Uwezo wa mwanamume kutafakari mambo upo kwenye misuli mikubwa zaidi kuliko mwanamke, mwanamke yeye ana sehemu kubwa ya kufikiria jambo lakini hana misuli kwenye kufanya uamuzi.

"Mwanamume hana nguvu kubwa kwenye kutafakari mambo, yeye yupo kwenye hatua ya kufikia hitimisho la jambo ndio maana mtoto wa kike akifukuzwa shuleni kwa sababu ya kukosa ada, anawaza atafeli, wakati mvulana anafikiria akimbilie wapi apate ada.

"Pia wanawake wanaongea zaidi kwa sababu ya nguvu za kihisia kwa kuachilia mambo kwa wepesi kuliko wanaume. Mwanamume anapotafakari jambo, huumiza na mifumo mingine ya kibaiolojia, anapoanza kuumiza akili huwa anaubebesha kazi ubongo, anapoutumikisha ubongo kutafuta majibu, anaathiri mifumo mingine.

"Kumbuka kwamba ubongo unachukua sehemu kubwa ya Oksijeni, unatafakari mambo magumu kwa mfano malezi, uhusiano. Unapochukua nguvu kubwa kutafakari, mfumo wa upumuaji unaendelea kushirikiana na mfumo wa mzunguko wa damu kugawanya kiwango cha Oksjeni kwenda kufanya kazi.

"Nguvu ya uchokaji wa ubongo kutokana na nguvu ya mashinikizo yaliyo nje kwenye mifumo ya kijamii inamtesa zaidi mwanamume kuliko mwanamke," anafafanua.

Msaikolojia Tiba huyo pia anasema mwanamume kwa tamaduni za Kiafrika anaonekana ndiye mtoaji wa vitu vyote kuhakikisha anapambana ili asipate aibu.

"Hawezi kushirikisha kwa urahisi jambo linalomtatiza kwa sababu anakimbia kupata aibu, anajikuta katika hali ya kubeba vitu vingi kwa wakati mmoja na kushindwa kutoa ili kupata nafasi ya kuweka vingine kufanya kazi kwa urahisi, wanaume wengi wanaingia kwenye hali hii ambayo inasababisha msongo wa mawazo na kutafuna nguvu za kiutendaji.

"Ili kujificha kwenye shida anayoipata, anakwenda kwenye tabia hatarishi za kutumia pombe, sigara na vitu vingine vya kuharibu zaidi mifumo ya kimwili. Kama ni maini, yanachuja sumu nyingi na baadaye yanapata athari kutokana na kemikali zinazopatikana na kupunguza uwezekano wa huyu mtu kuendelea kuishi.

"Wanaume wengi wanashindwa kujizuia kwenye kupata tendo la ndoa na hawazingatii ulaji ili kufanya kazi kwenye ubora wa kuzalisha madini mengine, wanajikuta virutubisho vingi wanapoteza kuliko ambavyo wanaingiza.

"Wengine wanafanya mazoezi magumu au maisha wanayoishi wanashughulisha zaidi mwili. Kwa mfano, kwenye afya ya mwili tunasema binadamu ana misuli ambayo inahitaji glukosi nyingi inayotoka kwenye stoo ndogo ya ini. Kama huli vyakula ili kuzalisha glukosi unapoteza nguvu ya misuli hadi baadhi ya viungo kuanza kupata shida," anafafanua.

**NINI KIFANYIKE?**

Msaikolojia Mwamnyanyi



Msaikolojia Tiba, Geofrey Mwamnyanyi (aliyesimama) akiwa kazini

anasema suala la wanaume kujiona wanapaswa kufanya kila kitu pamoja na nguvu ya kibaiolojia linafungwa kwenye malezi.

"Tunasema binadamu kuanzia mwaka 0-14 anakuwa kwenye kipindi cha kupokea vitu kama vilivyo hana nguvu ya kuvichuja, yaani atake asikitake vinaingia kama vilivyo, kama ambavyo umejifunza lugha yako ya kwanza kwa kuiga na mazingira.

"Binamu anafanya makosa mengi kuanzia miaka 22 hadi 32, anapofika miaka 40 hadi 45 ni kipindi cha kuziba maeneo ambayo ulikosea. Wanaume tukipata familia yenye watoto wa kiume kwanza wajengewe uwezo wa kujitambua unaozingatia mifumo yote ya afya.

"Wanaume wawe na nguvu ya kushirikisha kwa kuwa husaidia, tukijua na jamii ambayo inajijenga yenyewe bila maelekezo ngazi ya familia tutaendelea kuwa na watu ambao tumekuwa nao wanafikiri ni bora lakini wametengeneza matatizo kupitia fikra zao.


"Kama tunataka kupunguza vifo tuwajengee vijana au watoto wa kiume uwezo wa kumudu hali zote za kimazingira. Tukifanikiwa tutapunguza hali hiyo kwa vizazi vijavyo," mtaalamu huyo anasema na kushauri jamii iwe na makongamano mengi ya kuwafanya wanaume kujitambua na kuacha kufungwa na mifumo 'inayowatafuna'.

**KUTOKA NBS**

Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) kupitia ripoti yake ya 'Tanzania in Figures 2021' ya mwaka 2021, inaonesha wanaume nchini sasa wanaishi kwa wastani wa miaka 63.7 huku wanawake wakiwa na wastani wa miaka 69, ikiwa ni tofauti ya miaka 5.3.

Takwimu za NBS za miaka ya nyuma (2002 na 2012) zote zinaonesha wanawake waliongoza kuishi umri mrefu zaidi kulinganishwa na wanaume nchini. Mwaka 2002 utofauti kati ya makundi hayo ulikuwa miaka mitatu, mwaka 2012 ulipanda hadi minne na mwaka 2021 umefika miaka 5.3.

Ripoti ya NBS inaonesha mwaka 2002, wanaume walikuwa na wastani wa kuishi miaka 47 huku wanawake wakiwa na wastani wa miaka 50 na mwaka 2012 wanaume waliishi kwa wastani wa miaka 59.8 na wanawake walikuwa na wastani wa miaka 63.8.




Wastani wa umri wa kuishi Tanzania. **CHANZO: NBS Oktoba 3, 2022**

**WHO & UTAFITI**

Daktari wa Binadamu, Robert Shmerling ambaye ni Mhariri Mwandamizi wa Harvard Health Publishing huko Marekani, anasema kuwa kupitia utafiti wao wa mwaka 2020, wamebaini watu wanaoishi muda mrefu zaidi duniani, pamoja na mambo mengine, wanajiepusha na matumizi ya vileo, tumbaku na kupunguza ulaji wa nyama nyekundu.

Anasema nyama yenye shida kubwa ni ile yenye mafuta mengi, nyama choma iliyoungua na ile iliyosindikwa ambayo huchangia magonjwa ya moyo, kiharusi, kisukari na saratani ya utumbo kutokana na uzalishaji wa kemikali zinazodhuru afya.

Dk. Shmerling anarejea ripoti ya Shirika la Afya Duniani (WHO) ya mwaka 2020 inayobainisha kuwa asilimia 57 ya watu wote duniani wenye umri wa kuanzia miaka 65 ni wanawake, pia asilimia 67 ya watu wote duniani wenye umri wa kuanzia miaka 85 ni wanawake.

"Kwa Marekani, wanawake wanaishi wastani wa miaka mitano zaidi ya wanaume. Duniani, takwimu za WHO zinaonesha wanawake wanaishi wastani miaka saba zaidi ya wanaume," anawasilisha Dk. Shmerling, akishauri watu, hasa wanaume kupata mapumziko ya kutosha baada ya kazi ngumu kila siku, kufanya mazoezi na kula chakula cha asilia cha mimea kama mboga za majani na matunda kwa wingi.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## *Panguapangua ya makamanda ilete mabadiliko yanayostahili*

**MKUU** wa Jeshi la Polisi nchini, Inspekta Jenerali Camillus Wambura, amekuwa akifanya mabadiliko mbalimbali yakiwamo kuwahamisha baadhi ya makamanda wa mikoa kwenda makao makuu kuimarisha utendaji katika vitengo nyeti.

Sambamba na uhamisho huo, katika pangua pangua hiyo ambayo juzi ilifanyika kwa mara ya tatu tangu alipoteuliwa kushika wadhifa huo miezi kadhaa iliyopita, Wambura alimwondoa katika wadhifa aliyekuwa Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani nchini, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Willibrod Mutafungwa na kumpeleka kuwa Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mwanza. SACP Ramadhan Ng'anzi aliyekuwa Kamanda wa Mkoa wa Mwanza, ndiye ameteuliwa kubeba mikoba ya Mutafungwa.

Taarifa ambazo zimekuwa zikitolewa kila yanapofanyika mabadiliko hayo, zimekuwa zikibainisha kuwa mabadiliko hayo yanalenga kuimarisha utendaji ndani ya taasisi hiyo nyeti iliyopewa dhamana ya kulinda usalama wa raia na mali zao.

Mabadiliko ya mara kwa mara yanayofanywa na wakuu wa jeshi hilo kwa miaka mingi, yamekuwa yakielezwa kuwa yanalenga kuimarisha utendaji. Pamoja na kuelezwa hivyo, hali ya kiutendaji ndani ya polisi imekuwa ikiendelea kudorora mara kwa mara ikiwamo kulalamikiwa kuhusu mambo mbalimbali.

Miongoni mwa mambo ambayo jeshi hilo limekuwa likitwishwa lawama ni kubambikia wananchi kesi, watuhumiwa wa kesi mbalimbali kufariki dunia wakiwa mahabusu, baadhi ya askari kujihusisha na uporaji na ujambazi na rushwa hasa kwa askari wa usalama barabarani. Pia katika siku za karibuni, kumekuwa na ongezeko la ajali za barabarani, huku moja ya sababu ikiwamo kikosi cha usalama barabarani kushindwa kuchukua hatua madhubuti kudhibiti matukio hayo.

Kutokana na kuwapo kwa tuhuma na lawama hizo dhidi ya jeshi hilo, Rais Samia Suluhu Hassan katika mkutano wa maofisa na wakuu wa polisi, aliwataka kujitafakari juu ya mienendo hiyo ikiwamo baadhi ya askari kupangiwa trafiki, hivyo jamii kujiuliza kulikoni katika kikosi hicho?

Ni dhahiri kwamba hata mabadiliko aliyoyafanya Rais Samia kwa kumteua Wambura kuongoza jeshi hilo, kwa kiasi kikubwa yametokana na nia ya dhati katika kutekeleza yale aliyoyasema kwenye mkutano na makamanda na wakuu hao juu ya kujitathmini na kubadilika kiutendaji.

Kwa msingi huo, IGP Wambura katika mabadiliko ambayo anayafanya, inawezekana yana nia ya dhati ya kuleta utendaji wenye weledi ili kulirejesha jeshi katika taswira inayotakiwa baada ya kuchafuliwa na askari na maofisa wasio waaminifu.

Katika Kikosi cha Usalama Barabarani, kwa mfano, mabadiliko yaliyofanyika kwa kumwondoa Mutafungwa na kumweka Ng'anzi, kwa kiwango kikubwa yana nia ya kweli ya kusafisha hali ya hewa iliyozoeleka miaka nenda rudi hasa kukithiri kwa ajali na kutamalaki kwa rushwa na uonevu.


Vile vile, kupanguliwa kwa makamanda wa mikoa ni dhahiri askari na maofisa wamekuwa sehemu ya kulichafua jeshi kwa kuendekeza rushwa, kubambikia kesi, kupiga watuhumiwa na kuwaumiza hata kuwasababishia ulemavu wa kudumu na vifo.

Kwa ujumla, mabadiliko yanayofanywa mara kwa mara tangu Wambura ateuliwe kuongoza jeshi hilo, yanapaswa kuleta mabadiliko kiutendaji na kulirejeshea heshima jeshi hilo.

Walioteuliwa watambue kuwa imani ya wananchi dhidi ya jeshi hilo imepungua, hivyo wana kazi kubwa ya kumsaidia IGP Wambura kuleta tija kiutendaji na kurejesha imani hiyo na kuwafanya waone ni kimbilio kila wanapopata matatizo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

## *Rushwa hii ikomeshwe wanawake wastawi katika siasa*

**MOJA** ya mambo ambayo yamekuwa yakitajwa kukwamisha wanawake na kuwafanya washindwe kufikia malengo ya kupata nafasi mbalimbali za uongozi, ili kushiriki katika ngazi za uamuzi ni rushwa ya ngono.

Licha ya kuwapo kwa jitihada mbalimbali zinazofanywa na serikali na wadau wengine, kwa ajili kukomesha rushwa hiyo, ili kumnyanyua mwanamke, inaelezwa kuwa bado inaendelea kuwa kikwazo.

Miongoni mwa jitihada hizo ni kuwapo kwa makongamano, warsha na semina ambavyo hufanyika ili kuwahamasisha wanawake na kuwafundisha mbinu za kuwawezesha kuepuka rushwa hiyo, lakini hali haijatulia.

Kuendelea kuwapo kwa rushwa hiyo kumewaibua baadhi ya wadau ambao sasa wanasema kuna haja ya kuiundia kitengo maalum cha kuishughulikia, ili kupata mwarobaini wa kuikomesha.

Wadau wa kutetea haki za wanawake wanashauri rushwa hiyo isijumuishwe na rushwa nyingine, badala yake iundiwe kitengo maalum katika Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum.

Ni katika mafunzo ya kuongeza ushiriki wa wanawake, katika nafasi za maamuzi na mbinu za kufanya ujasiriamali yanayoendeshwa na Kituo cha Sauti ya Jamii Kipunguni, jijini Dar es Salaam, wanapaza sauti zao kuhusu kukithiri kwa rushwa hiyo.

Mafunzo hayo yanaendeshwa na Kituo cha Sauti ya Jamii Kipunguni jijini Dar es Salaam, ili kuwaandaa wanawake kushiriki kwa wingi katika uchaguzi wa serikali za mitaa na uchaguzi mkuu wa mwaka 2025.

Inaelezwa kuwa visa na mikasa vinavyosimuliwa na baadhi ya wanawake katika mafunzo hayo, ni kwamba baadhi yao wanakiri wazi kwamba walishatoa rushwa hiyo baada ya kubanwa na mazingira na kuamua kujirahisisha ili wafanikiwe kupata kile wanachohitaji.

Ninaungana na wadaau hao kuwa utoaji wa rushwa hiyo umekuwa ukiibua mijadala, huku wanawake wakilaumiwa bila kufanya uchambuzi wa kina, ili kujua chanzo cha kuendelea kuwapo kwa rushwa hiyo.

Rushwa hiyo inadhalilisha utu wa mtu, na sidhani kwamba kuna mwanamke ambaye kwa ridhaa yake anaweza kudhalilisha utu wake bali vikwazo anavyowekewa vinaweza kuwa chanzo cha rushwa.

Hivyo, wazo lao la kutaka rushwa hiyo itenganishwe na rushwa nyingine, ninadhani liko sahihi, kutokana na ukweli kwamba wanafanya hivyo bila kukubali wao, bali ni kwamba hujikuta wamebanwa.

Wadau hao wanatamani mfumo wa utoaji haki, utazamwe upya, kwa kuwa wanabainisha kwamba ingawa bosi katika siasa au ofisini anaweza asitamke wazi kuitaka rushwa hiyo, mazingira yanaweza kuonyesha kuwa anaitaka.

Mojawapo ya mazingira hayo ni kuzungushwa kutatuliwa tatizo au kuzuia jina wakati wa kuomba uongozi, hali ambayo inaelezwa husababisha baadhi ya wanawake kujikuta katika mtego wa kujipeleka na kutoa rushwa.

Kimsingi, mazingira hayo yanaumiza kusikia mwanamke amepata nafasi ya uongozi kwenye chama baada ya kuombwa rushwa ya ngono na kutoa au amejirahisisha mwenyewe ili apate nafasi anayotaka.

Hivyo, ninadhani rushwa hiyo ikiundiwa kitengo maalum cha kuichunguza kama wadau hao wanavyoshauri, wanaojipeleka au kujidhalilisha, lengo lao ni nini, badala ya kuwanyooshea vidole na kumbe wanabanwa na mfumo.

Ikumbukwe, TAKUKURU inatambua kuwa mtoa rushwa na mpokea rushwa, wote wana makosa, lakini kwa suala la rushwa ya ngono, kuna upande ni kama unalazimishwa kufanya hivyo huku ukidhalilika.

Ni vyema rushwa hiyo ingechukuliwa kama udhalilishaji wa utu wa mtu, vinginevyo, wanawake wanaweza kubaki katika nafasi za viti maalum kwenye siasa, badala ya kusimama na kupambana na wanaume majukwaani.

SAFU

FIKRA MBADALA

# Uandaliwe utaratibu maalumu wa kiprotokali



Pascal Mayalla

KWA Maslahi ya Taifa, leo inajikita kwenye masuala ya kiprotokali. Tanzania tuna protokali za viongozi wetu mbalimbali zikiwamo za mke wa Rais ajulikanaye kama 'First Lady'.

Sisi Tanzania tangu tumepata uhuru, tumekuwa na marais wanaume, hivyo siku zote tumekuwa na protokali ya mke wa rais, yaani First Lady. Kutokana na siku zote Rais kuwa mwanamume, protokali iliyopo ni mke tu wa Rais, yaani First Lady.

Tena kwa vile tumetawaliwa na wakoloni Waingereza, nchi yao ni nchi yenye dini ya Anglikana, hivyo kiserikali ya Uingereza inatambua mke mmoja tu, hivyo hata protokali ya First Lady ni kutambua mke mmoja tu. Akitokea rais ana wake wawili, kama ilivyokuwa kwa Rais wa Awamu ya Pili, Mzee Ali Hassan Mwinyi, wake zake Bi Khadija na Mama Siti, protokali ya First Lady, ilimtambua mke mmoja tu.

Kwa vile nchi yetu haina dini, ila watu wake wana dini zao, kwa nini tukumbatie protokali za wakoloni za mke mmoja? Akitokea rais ana wake wawili, kwa nini protokali imbague mke mmoja kuwa 'First Lady' na kumwacha yule mwingine? Kwa nini tusiunde protokali yetu, akitokea Rais ana wake wawili, tuandae tuwatambue wake wote wawili! na akitokea Rais ana wake wanne, wote watambuliwe kama ma-First Lady 1,2,3 4 na akitokea rais wetu ni mtu mwenye dini ya asili kama Chifu Burito, wake wote wa rais wanakuwa ni ma First Ladies. Mbona hili hapo kwa jirani zetu Eswatini (Swaziland) kwa Mswati limewezekana? Kwa nini tuendelee kukumbatia protokali za kikoloni?

Tukija kwa protokali ya mwenza wa rais, hakuna aliyewahi kuwaza kuwa kuna siku Tanzania inaweza kuwa na Rais mwanamke, hivyo ilivyotokea kwa kudra za Mwenyezi Mungu, sasa tuna rais mwanamke, Mama Samia Suluhu Hassan, protokali bado zinamtambua mke wa Rais, sijabahatika kusikia protokali yoyote ya mume wa rais wala kusikia akitajwa popote kufanya lolote. Watu wa protokali walibidi wajiongeze Rais akiwa mwanamke waje na protokali ya mume wa Rais kaka 'First Gentleman'. Wakati wa shughuli zozote za kitaifa, nafasi ya 'First Gentleman' iwapo na hata rais akifanya ziara za kiserikali, waandamane.

Kumbe nchi ikiwa na rais mwanamke, kiitifaki inakuwa haina First Lady. 'First Ladies' wa Afrika wana taasisi yao na hivi karibuni imefanya kongamano la wiki nzima Bujumbura nchini Burundi. Kwa vile sasa Tanzania tuna Rais mwanamke, hatuna First lady, hivyo Tanzania iliwakilishwa na mmoja wa 'first ladies wa awamu zilizopita.

Nimebahatika kuhudhuria kongamano hilo kama mwanahabari, 'First Lady' wetu akapokewa nchini Burundi kwa protokali ya ki- 'first lady', tangu mwanzo hadi mwisho, tukabahatika kupanda ndege moja.

Tulipofika ile nchi ya kubadilisha ndege, flights mimi mwananchi napita sehemu ya abiria wa kawaida, nashangaa kukutana na 'first lady' wetu anahudumiwa kama abiria wa kawaida wakati alipaswa kuwa na hadhi ya watu mashuhuri (VIP).

Nikasukumwa na uzaendo kuwaelekeza wenyeji wetu pale kuwa yule mnayemwona pale ni 'first lady' wetu. Jamaa wakashituka na kuanza kukimbizana kumchukua kutoka kwa abiria wa kawaida na kumpeleka VIP.

Kubwa kuliko ni tulipofika nyumbani. Nikajua kwa vile kule ni ugenini hawakuwa na taarifa za ujio wa 'First Lady', lakini hapa nyumbani napo!. Yale yale ya kule na huku nyumbani kila mtu anamtambua fulani ni 'fast lady' wetu wa awamu iliyopita, iweje asipokelewa ki- VIP?

Watu wetu wa itifaki inawabidi kujiongeza. Hata kama Tanzania kwa sasa haina 'First Lady' rasmi, tufanye yafuatayo;-

- Teweke protokali ya mwenza wa Rais. Rais akiwa mwanamume, mkewe au wakeze watambuliwe kama 'First Lady'. Rais akiwa mwanamke, iwapo protokali ya 'First Gentleman'.
- Ikitokea mmoja wa 'first ladies' wa marais wa awamu zilizopita amealikwa nje ya nchi kama 'first lady', apatiwe protokali ya ki 'first lady' toka nyumbani. Kwa maana hiyo apewe heshima kama 'first lady', asafiri kama 'first lady' na kupokewa kama 'first lady'.

Kwa mujibu wa katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Tanzania ni nchi moja yenye sehemu mbili, Tanzania Bara na Tanzania Visiwani. Zanzibar si nchi bali ni sehemu ya JMT yenye utawala wake wa ndani. Katiba ya JMT inatambua Rais wa Zanzibar na Waziri Kiongozi tu.

Mabadiliko ya katiba ya Zanzibar ya 2010 yaliyounda Serikali ya Umoja wa Kitaifa, yameitangaza Zanzibar kuwa nchi, ni moja ya nchi mbili zinazounda JMT. Nafasi ya Waziri Kiongozi imefutwa na kuna makamo wawili wa rais. Katiba ya JMT haiyatambui mabadiliko hayo, lakini watu wa protokali wamejiongeza, hao makamu wawili wa Rais kutoka Zanzibar wakija Bara, wamewekewa protokali yao mahususi.

Kwa mantiki hiyo, hata Rais akiwa mwanamke hii inakuwa haina 'First Lady', 'First Ladies' wote wa nyuma, wakialikwa popote, waandaliwe itifaki yao badala ya kuheshimika kuwa ni 'first lady' ugenini akirudi nyumbani anageuka mwananchi.

**Wasalaam.**
**Paskali**
**+255 754 270403**

MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Watanzania tuwe makini 2025 au 2030



Na Joseph Kulangwa

WATANZANIA ni watu wenye mshikamano na umoja wa dhati na katika kuthibitisha, wanapopatwa na matatizo ndipo utaona wanavyokuwa wamoja na kushirikiana.

Mfano mzuri ni mwaka 1978 majeshi ya Uganda chini ya Meja Jenerali Idi Amin Dadah yalipovamia ardhi ya Tanzania kupitia mpaka wa Mutukula mkoani Ziwa Magharibi (leo Kagera).

Baada tu ya Rais, Mwalimu Julius Nyerere kulitangazia Taifa: "Sababu ya kumpiga tunayo! Nia ya kumpiga tunayo! Na uwezo wa kumpiga tunao!", Watanzania walishikamana kwenda mstari wa mbele kuikomboa ardhi iliyotwaliwa na majeshi ya Nduli.

Wako waliojitolea binafsi kwenda kupigana ana kwa ana na majeshi hayo, wako waliojitolea fedha na mali zao ikiwa ni pamoja na magari na wanyama ili mradi ushindi upatikane na ukapatikana kweli.

Hao ndio Watanzania ambao leo pamoja na matatizo waliyo nayo, bado wameshikamana licha ya tofauti ndogo ndogo. Wako nyuma ya Rais wao Samia Suluhu Hassan, kukabiliana nayo kwa mustakabali mwema wa taifa lao.

Siri yake ni nini? Siri kuu ni kiongozi waliye naye, Samia, Rais huyu wa sita wa Tanzania, amejinasibisha kweli ni kiongozi anayependa watu wake, anafanya kila analoweza, kuhakikisha nchi inasonga mbele kwa utulivu, amani, upendo na umoja.

Hili Watanzania wanatakiwa kulishukuru kutokana na kudra za Mwenyezi Mungu. Inawezekana uongozi ungekuwa bado chini ya Rais wa tano, Dk. John Magufuli pengine mambo yangekuwa yameshagota na tunalia kilio cha mbwa.

Kwa nini? Dk Magufuli yawezekana alikuwa na nia njema kabisa na nchi yake, ndiyo sababu alikuwa anakwenda kasi ambayo kama nchi ingejikwaa ingeangukia pabaya sana. Maagizo na utekelezaji yalikuwa yanakimbia kuliko mbio za watu wake. Haraka haraka isingekuwa na baraka kabisa. Hapa hapatoshi kuyasema yote.

Jambo la msingi kwa Watanzania, ni kuona fursa zilizopo chini ya uongozi wa Rais Samia na kufikiria cha kufanya mwaka 2025 kuhusu suala la nani aiongoze Tanzania kuanzia hapo, CCM wenye Samia wao wameshajitanabahisha kumsimamisha.

Kilichobaki ni kwa Watanzania wengine wa kila itikadi nao kuamua hasa kwa kuzingatia haya anayoyafanya hivi sasa kwa nchi na watu wake bila kujali itikadi zao. Kosa likifanyika 2025, bila shaka itakuwa bahati mbaya sana kwa Watanzania.

Historia ya nchi hii inatufunza mengi kwamba kumekuwa na kupokezana vijiti kwa uongozi wa juu kitaifa na kuingia viongozi wanaotofautiana hulka, akili, tabia na matendo, hivyo baada ya Samia atakuja Rais mwenye utofauti.

Ikumbukwe historia kuwa kama Mwalimu Nyerere asingeng'atuka 1985, ina maana angeongoza nchi mpaka Oktoba 14, 1999. Ni dhahiri Watanzania walishamwachia Mwalimu nchi aongoze mpaka achoke ndiyo sababu akagundua na kuondoka.

Na baada ya kung'atuka, ndipo ukaja utaratibu wa zamu kati ya Tanzania Bara na Zanzibar katika kutoa viongozi; kwamba awamu hii akitoka Zanzibar basi ijayo atoke Bara, na akitoka Bara basi Makamu atoke Zanzibar na kinyume chake.

Lakini kulikuwa na zamu ambayo haikuwa dhahiri, ingawa ilitekelezwa, kwamba awamu hii akiongoza Mwislamu basi ijayo aongoze Mkristo. Ilijipanga yenyewe. Hiyo inaendelea hadi leo. Kama nilivyosema awali, Mwalimu Nyerere ambaye angeongoza mpaka 1999, angepata fursa angeacha wosia wa nani afuate.

Hakika, angeacha majina ya watu wawili; Edward Sokoine (Bara, Mkristo) na Dk Salim Ahmed Salim (Visiwani, Mwislamu). Lakini kutokana na lile la Rais afuataye atoke Zanzibar, bila shaka Dk. Salim angemrithi. Lakini kwa kuwa aliondoka 1985, ndiyo sababu Alhaji Ali Hassan Mwinyi akachukua hatamu kwa kuwa alitoka Zanzibar.

Rais Mwinyi alipomaliza ngwe yake 1995, Nyerere akawa na majina mawili, Dk. Salim na Benjamin Mkapa, lakini kutokana na zamu ya eneo na dini, Mkapa akafaa. Baada ya Mkapa, utaratibu wa zamu ya maeneo ukafa lakini wa dini ukabaki. Akaingia Dk Jakaya Kikwete.

Baada ya Kikwete akaingia Dk. John Magufuli, akafuata Samia. Hivyo atakayekuja baada ya Samia, atakuwa Mbara lakini pia Mkristo. Tukichambua kwa kina, kwangu mimi nabaini kuwa katika zamu hizo, ukitazama Wakristo walikuwa viongozi jeuri, kuanzia Mwalimu, Mkapa na Magufuli, lakini Waislamu walikuwa rahimu sana, sina haja ya kutaja lakini ni dhahiri.

Hivyo, nasema tukifanya makosa ili 2025 aje mwingine, ataingia jeuri na hata tukivuta mpaka 2030 atakuja jeuri na inawezekana akamzidi JPM. Kazi kwetu. Alamsiki!

***kulangwasos@gmail.com**

# Miradi ya afya yampasua kichwa RC

**Na Gurian Adolf,** SUMBAWANGA

Mkuu wa Mkoa wa Rukwa, Queen Sendiga, ameiagiza Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kufanya uchunguzi kwenye miradi ya afya inayotekelezwa katika Manispaa ya Sumbawanga ili kubaini thamani ya fedha.

Agizo hilo alilitoa jana alipofanya ziara ya kukagua ujenzi wa vituo vya afya Mollo unaogharimu Sh. milioni 400, Matanga Sh. milioni 500, Zahanati ya Nambogo, Mponda Sh. milioni 80 na hospitali ya wilaya iliyoko eneo la Isofu ambayo ujenzi wake unagharimu Sh. bilioni 1.8.

Sendiga alisema pamoja na serikali kutoa fedha hizo kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hiyo, alieleza kutoridhishwa na thamani ya miradi hiyo.

"Nawaagiza TAKUKURU Wilaya ya Sumbawanga siku ya Jumatatu Oktoba 24 kuwasilisha ofisini kwangu taarifa ya kina kuhusu hatua walizochukua tangu ilipoanza kutekelezwa miradi hiyo kwani imechelewa kukamilika tofauti na muda uliokusudiwa," alisema.

"Wajibu wetu ni kusimamia kazi katika maeneo ambayo Rais Samia hawezi kufika. Sisi viongozi wa mkoa na wilaya tutumie nafasi zetu kutatua kero za miradi ya afya ili wananchi wapate huduma kwa wakati," alisisitiza.

Mkuu wa Wilaya ya Sumbawanga, Sebastian Waryuba, alisema atahakikisha miradi hiyo inakamilika kwa wakati na thamani ya fedha za serikali zilizotolewa zinaleta matokeo chanya.

Naye Meya wa Manispaa ya Sumbawanga, Justin Malisawa, alisema ujenzi wa zahanati ya Mponda ulioanza mwaka 2013 kutokamilika kwa wakati, alisema halmashauri hiyo itatoa Sh. milioni 25 zitakazokamilisha ujenzi huo mapema mwakani.

Sendiga hivi sasa yuko katika ziara maalumu ya kukagua miradi ya afya inayotekelezwa mkoani hapa ili kubaini changamoto zilizosababisha miradi hiyo kutokukamilika kwa wakati sambamba na kuona thamani ya fedha katika miradi hiyo.



Meneja wa Wateja Maalum, Tigo Pesa, Mary Ruta (kushoto), akikabidhi zawadi ya vifaa vya nyumbani kwa Rashmy Abdilahi Bampara mkazi wa Tabata, aliyeibuka mshindi wa droo ya wiki ya tatu ya promo ya Twenzetu Qatar na Hisense, jijini Dar es Salaam jana. Kulia ni Ofisa Masoko wa kampuni ya Hisense, Joseph Mavura. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wavamizi vyanzo maji waamuriwa kuondoka

**Na Christina Haule,** MVUHA

SERIKALI mkoani Morogoro imetoa siku mbili kwa wafugaji waliovamia na kuharibu vyanzo vya maji katika bonde la maji Wami Ruvu kuondoka kwa hiyari kabla ya kuondolewa kwa nguvu.

Akizungumza kwenye kikao kilichowakutanisha wafugaji, ofisi ya bonde la Wami Ruvu, maliasili na viongozi wa serikali, kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Morogoro Fatma Mwasa, Mkuu wa Wilaya ya Morogoro, Albert Msando, alisema licha ya malalamiko ya wafugaji juu ya kuwa na sheria zao za vijiji zinazowaruhusu kutumia vivuko kunyweshea maji mifugo yao, sheria hizo hazizidi sheria za rasilimali za maji za mwaka 2009 na ya mazingira ya mwaka 2004.

Msando alisema sheria hizo haziruhusu shughuli zozote za kibinadamu kufanyika ndani ya mita 60 ya chanzo cha maji.

"Tumewapa wafugaji siku mbili yaani Jumamosi (jana) na Jumapili (leo) ili wajitafakari na kuondoka kwa hiari kwenye vyanzo vya maji na maeneo ya hifadhi. Hatuwezi kuruhusu mifugo ikaingia kwenye maeneo hayo huku tukiwatafutia taratibu zingine za kunyweshea zikiendelea kufanyika," alisema.

Mkuu huyo wa wilaya alisema pamoja na masuala ya kibajeti kwa kushirikiana na Bonde la Wami Ruvu wanaangalia namna ya kufanya ili kuchukua hatua za dharula kuokoa mifugo kwa sababu hawataki mifugo ife jambo ambalo litazua taharuki.

Msando alisema watachukua hatua zote muhimu kuhakikisha wanapata maji kwa ajili ya mifugo lakini si kwa kupeleka mifugo ndani ya vyanzo vya maji.

Hata hivyo, aliwataka wafugaji kuacha kulalamika bali kuona namna ya kutumia fedha zao kuongeza nguvu katika ujenzi wa miundombinu ya mifugo ikiwamo ujenzi wa malambo (mabirika ya kunyweshea maji).

"Mkikamatwa kwa kuingia kwenye vyanzo vya maji, mnatozwa faini ambazo wakati mwingine zinafika mpaka Sh. milioni nne kwa mfugaji mmoja. Sasa hapo utakuwa umejenga mabirika mangapi kama una moyo wa kujenga mabirika ya kunyweshea wakati birika moja mpaka linakamilika halizidi Sh. milioni moja? alihoji.

Awali, Mkurugenzi wa Bodi ya Maji Bonde la Wami Ruvu, Elibariki Mmassy, alisema kwa mujibu wa Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), hali ya mvua imepungua kwa sasa ambapo kulipaswa kuwe na mvua za vuli lakini zinatarajiwa kunyesha wiki ya tatu na ya mwisho ya Desemba jambo ambalo ni hatari na halilingani na kiwango cha maji kilichoko kwa ajili ya matumizi mbalimbali.

Mmassy alifafanua maji yaliyopo kwenye vyanzo ni asilimia 40 ya mahitaji yote ambapo mitoni kuna lita 4,000 wakati wastani wa matumizi maji ya majumbani ni lita 5,800.

Kutokana na hali hiyo, alisema bodi iliamua kuanza kukagua vyanzo vyake na kubaini uharibifu mkubwa unaofanywa na wakulima na wafugaji na kuamua kusitisha kufanya shughuli zozote kwenye vyanzo vya maji.

Alisema changamoto zote hizo zinasababishwa na mabadiliko ya tabianchi, huku kukiwa na ongezeko la kukithiri ukame ambao pia umeathiri shughuli za kilimo na ufugaji sambamba na kupungua kwa kiasi kikubwa cha kina cha maji kwenye mito mikubwa ikiwemo Mgeta na Mngazi ambayo yote kwa pamoja inapeleka maji Mto Ruvu baada ya mito hiyo kujaa mchanga.

Mmoja wa wafugaji, Timoth Olekoyesa aliiomba serikali kuwaruhusu kutumia vivuko vilivyotengwa kwenye mito hiyo kwa mujibu wa sheria ndogo za vijiji kunyweshea mifugo ili isife kwa kukosa maji kwa sababu wanaweza kupoteza mifugo mingi kwa wakati mmoja.

## Watakiwa kutoa maoni kuokoa maisha

**Na Beatrice Shayo**

WATANZANIA wameshauriwa kujisalimisha kwa kutoa maoni yao katika mjadala wa nishati ya kupikia kwa kutumia kuni na mkaa ili kuokoa afya za wananchi.

Kongamano hilo linatarajiwa kufanyika katika Ukumbi wa Julius Nyerere, Novemba 1 na 2, mwaka huu, na mgeni rasmi anatarajiwa kuwa Rais Samia Suluhu Hassan.

Akizungumza na Nipashe juzi, Waziri wa Nishati, January Makamba, alisema kwa sasa kinachoendelea ni uelimishaji kuelekea kwenye mjadala huo unaosubiriwa kwa hamu na Watanzania wote kwa ajili ya kuokoa idadi kubwa ya watu wanaopoteza maisha yao.

Makamba alisema watu wanapoteza maisha kutokana na sumu inayotokea kwenye kuni na mkaa wakati wote wanapoendelea na shughuli zao za mapishi katika nyumba zao.

Alisema maoni yao yataambatana na mahitaji ya watu wanaotaka kushiriki mjadala huo kujisajili kwa kupiga namba ya bure 0800750203 au mtandao kwa www.cleancooking.co.tz kwa lengo la kuchukua maoni yatakayoboresha wazo la Watanzania kuondokana kwenye nishati ya kuni na mkaa na kuhamia katika gesi kwa gharama nafuu nchini.

"Hii nchi ni yetu wote na kila mmoja mmoja anayo haki na wajibu wa kuboresha mambo haya ambayo serikali tunaamini idadi hii ya vifo vya akina mama wanaotumia kuni na mkaa kupikia itaondoka sambamba na kukuza uchumi wa kila mmoja," alisema Makamba.

"Nitoe rai sasa kila mtu mwenye nia ya kutoa maoni yake basi ajisajili kwa njia ya mtandao au kupiga simu ya bure apewe maelekezo kuelekea Novemba mosi na pili, huku tukio hilo likishuhudiwa na Rais wetu mpendwa, Samia Suluhu Hassan," aliisitiza.

Kwa mujibu wa takwimu za Wizara ya Afya, watu bilioni 2.4 duniani wanatumia nishati chafu zinazopelekea vifo vya watu bilioni 1.6 na Tanzania kati ya watu 30,000 hadi 45,000 hupoteza maisha kila mwaka.

# MAISHA

OKTOBA 23, 2022

Nipashe

Baba, Mama na Mwana

*Jumapili*





## Jipange vizuri katika kusafisha nyumba yako

Ukurasa 15



## Makaroni ya nazi

Ukurasa 14



## 'TURTLENECK' Sweta linalokupa burudani


Ukurasa 13




# TUMIA KARANGA MBICHI Kutengeneza uso unaovutia

Ukurasa 14

## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA






| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| ■ | T | A | M | K | O |
| ■ | A | ■ | ■ | A | ■ |
| U | M | A | ■ | N | ■ |
| ■ | B | ■ | U | D | A |
| ■ | U | ■ | ■ | I | ■ |
| S | A | N | D | A | ■ |

## AMSHA AKILI

TUMIA RANGI ZA NJANO, KIJANI NA NYEKUNDU KUPENDEZESHA MCHORO HUU



## TOA TOFAUTI 5




## FUMBO TOTO

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| ■ | | | | | |
| ■ | | ■ | ■ | | ■ |
| | | | ■ | | ■ |
| ■ | | ■ | | | |
| ■ | | ■ | ■ | | ■ |
| | | | | | ■ |

Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyopo wazi:
DAU, AMA, TAMBI, JAZWA, JAMBIA, WAKATI

## WATOTO

# PAKA RANGI







MTOTO Juma alikuwa akimsaidia mama yake kulima bustani ya mboga pembeni ya nyumba yao. Wakati wanalima Juma alimuuliza mama yake maana ya maneno aliyoambiwa na mwalimu wake.

Juma: Eti mama ni kweli mchuma janga hula na wakwao?

Mama: Ndio mwanangu, ni lazima watakula pamoja.

Juma: Kwani ni lazima kila anayechuma janga lazima ale na ndugu zake?

Mama: Mwanangu huo ni msemo unaomaanisha kila baya unalolitafuta, utaathirika pamoja na ndugu zako ni lazima kujiepusha.

**SWALI**

Taja matumizi tofauti ya chakula aina ya karanga

## MAISHA NDIVYO YALIVYO

Na Flora Wingia



# Mama afa kisa dharau za bintiye aliyemsomesha!

KARIBU tena msomaji wangu tuendelee na kisa cha binti daktari aliyemdharau mama yake akaishia pabaya. Wiki iliyopita tuliona mama yake alivyomtembelea, akamdharau na kumwambia hamtambui kwa madai kuwa hana wazazi, yaani mama wala baba, wala ndugu.

Akaingia zake ndani na kumwacha mama sehemu ya getini pamoja na walinzi kwani alikuwa ametokea kazini. Mama alivyoona yale madharau akaondoka japokuwa ilikuwa usiku.

Jirani akaona kanisa ikabidi aingie mle amwombe Mungu. Wakati anaomba akamjia Mchungaji wa lile kanisa na kumsemesha. Mama akamweleza yote aliyopitia na zaidi vile bintiye alivyomdharau. Mchungaji akamtia moyo. Hata hivyo mama akasema hana budi kuondoka.

Leo msomaji tuangalie kilitokea nini baada ya mama kuondoka pale kanisani. Mchungaji alimwambia asubiri akamgongee binti yake amwulize kulikoni. Mama akamkataza kwamba amwache tu lakini akasema anamwombea Mungu bintiye yasije yakamkuta mabaya kwani bado anampenda pamoja na hicho alichomfanyia.

Mama akasema hawezi kuendelea kukaa pale asije akamkufuru Mungu. Kwa kuwa binti yangu hataki kuiona sura yangu, inatosha baba mtumishi acha niende. Ilikuwa si rahisi mtumishi huyu kumruhusu aondoke usiku ule.

Ni kutokana na ukweli kwamba mama yule ni mgeni lakini akasema ili awe na amani ni bora aondoke eneo hili aende pengine. Hakuwa na namna ya kumzuia, akamtaka radhi mtumishi yule.

Kabla ya kuondoka akampatia Sh. 30,000/= akamwambia: ''Mama nakuombea, Mungu akutangulie na naona moyo wako umeachilia juu ya mtoto wako''.

Ni kweli aliachilia lakini maumivu ya moyo bado huenda yalikuwapo. Nikijaribu kuvaa viatu vya huyu mama, nakuta havinitoshi na hasa nikifikiria jinsi wazazi wanateseka na watoto. Alibeba mimba miezi tisa, baba hayupo, alifanya vibarua ale na kumsomesha binti yake.

Leo binti anamkataa mama yake , anakuwa ngangari, hageuki nyuma, anaendelea na maisha yake. Lakini mama amebaki na huzuni japo moyoni anasema ameachilia. Bado atakuwa na msongo wa mawazo akitafakari maisha yake.

Mume alifariki dunia yeye akiwa na umri miaka 22 na hakutaka kuolewa tena ili amtunze bintiye, lakini leo amefanikiwa hamtaki. Anamkana mbele za watu wakiwamo mabosi na marafiki zake kwamba hana wazazi. Binti akasahau malezi yote ya mama.

Mtumishi huyu wa Mungu akamwambia, mama sina neno kwa hayo uliyonieleza. Mchungaji wakati anasimulia kisa hiki alikuwa anajikaza kwani ni mengi wanakutana nayo kuhusu maisha ya watu. Akamwambia ningetamani uwe mama yangu kwani mamangu mzazi alitangulia mbele za haki miezi miwili iliyopita.

Mama akaondoka. Ile tu anavuka barabara, mama akagongwa na gari. Mchungaji akasikia mayowe ya mama fulani kagongwa na gari. Akakimbilia kuona hiyo ajali akakuta kumbe ni yule mama aliyekuwa anaongea naye muda mfupi uliopita pale kanisani.

Mtumishi huyu wa Mungu alilia sana, aliumia sana. Kwa haraka akachukua gari lake akamwingiza ndani na kumkimbiza hospitalini. Kumwangalia madaktari wakasema amepoteza damu nyingi sana aliumia sehemu ya kichwa, hawezi kuishi tena!

Mchungaji alilia sana akamwambia Mungu, kwa nini usingemrehemu tu aendelee kuishi hata na mimi. Lakini mama alikataa. Mama alikufa akiwa na mawazo ndani yake.

Kumbuka mama hakuwa na mwenyeji pale mjini. Yule kijana aliyemleta kwa binti yake hakuacha anwani yake anakoishi na wala mama hakusema kijiji anakotoka pengine ingekuwa rahisi kujua ndugu zake.

Mzigo ukamwelemea Mchungaji. Akampigia simu yule binti daktari akamjulisha kuwa mama yake mzazi amefariki dunia. Binti akahamaki kwenye simu akawa anataja neno mama mfululizo huku akionekana kama anatembea. Akawa anasema, mama, mama, mama hadi mchungaji akakata ile simu kwani alikuwa hamwelewi.

Si ajabu binti lile tukio la kumdharau mama pale getini na kumwambia kwamba hamtambui na wala asimsogelee, lilirudi akilini kwake na kumkumbusha kuwa yule uliyemkataa ndiye mama yako.

Lakini kama ndivyo, tayari alikuwa amechelewa kwani ile dharau hakustahili kumfanyia mama yule. Pengine angemsikiliza kwanza ajue sababu za kuja kumwona toka kijijini.

***Msomaji wangu, Maisha Ndivyo Yalivyo. Nilidhani ningemaliza leo lakini wiki ijayo usikose nitaeleza nini kilimtokea dada daktari baada ya taarifa msiba wa mama yake. Una maoni, kisa? Ujumbe 0715268581.***

## NAWAZA KWA SAUTI

Na Salome Kitomari



# Hali ya hoteli zinazohudumia wasafiri Morogoro si ya kuridhisha

UNAPOSAFIRI kwenda mikoa ya Nyanda za Juu Kusini, Kanda ya Kati na Ziwa lazima utapita mkoani Morogoro na kwa wanaotumia magari ya alfajiri kama wanaokwenda Songea, Njombe, Mbeya na Ruvuma lazima wanasimama kunywa chai.

Kwa wale wanaokwenda Mwanza, Musoma, Shinyanga, Bukoba, Kahama na kwingine kwa mwelekeo huo, wanapotoka Dar es Salaam kituo cha kwanza ni mkoani humo kwa ajili ya kupata chai ya asubuhi.

Kama haitoshi wanaoenda mikoa ya jirani kama Dodoma hasa kwa magari yasiyo ya alfajiri lazima wanasimama kupata chakula cha mchana au jioni kwenye moja ya hoteli za mkoa huo kutegemeana na makubaliano baina ya dereva na wamiliki wa hoteli.

Kwa ujumla, unaposafiri kwenda mikoa mingine hususan ya Kanda ya Kaskazini na Kusini, huduma za vyakula ni za kuridhisha sana kuanzia usafi wa eneo husika na vyakula lakini si kwa njia ya Morogoro.

Hoteli zote ambazo mabasi yanasimama ili abiria wachimbe dawa, wapate huduma ya chakula na mapumziko kwa ujumla si za kuridhisha kabisa hali inayozua maswali mengi kwa Manispaa ya Morogoro kwamba huwa haioni hayo yote?

Kuanzia vyoo ni vichafu na vibovu kiasi kwamba asilimia kubwa ya wasafiri huishia kupata maradhi tu kwa kuwa hakuna anayefuatilia bali mwenye biashara huamua kukifanyia anavyotaka kwa kuwa hakuna ukaguzi.

Vyakula vinavyouzwa bei ya ulanguzi havina thamani ya fedha bali wizi kwa wasafiri kwa kuwa watu wanauziwa ilimradi wakati mwingine havijaiva, havijaandaliwa vizuri viko ilimradi kiasi kwamba inazua maswali serikali haioni haya yote?

Pia vinywaji vinauzwa mara mbili hadi tatu ya bei na wakati mwingine abiria ananunua kwa kuwa anahitaji na ndilo eneo alilofikishwa na dereva wa gari husika.

Wakati mwingine ni sawa bei wanazouza kama zingeendana na uhalisia kwamba chakula kimeiva vizuri, eneo linaridhisha kwa usafi na mwonekano sahihi, kuliko hali ilivyo sasa.

Ninatambua kwenye kila mamlaka ya serikali za mitaa kuna ofisa afya, ambaye moja ya majukumu yake ni kufuatilia usafi wa maeneo yote ya biashara hasa hoteli na migahawa inayotumiwa na watu wengi kisha kuchukua hatua hata ya kufunga kwa ambaye hajakidhi vigezo.

Migahawa na hoteli ninayoizungumzia mjini Morogoro iko kilomita chache kutoka iliko Manispaa ya Morogoro. Swali ninalojiuliza wanafanya ukaguzi hadi kwenye vyoo, wanaona vingine havina milango na ni chakavu kupita kiasi au wanaacha bora liende na kukusanya kodi pekee?

Ni muhimu sana Manispaa ya Morogoro ikajali afya za wananchi kama ambavyo maeneo hayo yanawaingizia fedha kama chanzo cha mapato basi wanao wajibu wa msingi kufuatilia huduma zinazotolewa humo kama zinaridhisha.

Ni lazima hatua zichukuliwe mazingira ya hoteli na migahawa iboreshwe au kujengwa upya kama mtu anataka kuwekeza kwenye huduma hizo afanye uwekezaji wa kuridhisha na kukidhi vigezo vyote vya afya kuliko wananchi kuingizwa kwenye matatizo.

Kama maeneo haya wanatoza fedha zaidi ya bei halisi ya bidhaa husika,kwanini wanashindwa kuboresha maeneo yakawa mazuri na ya kuridhisha kuanzia huduma za vyoo,chakula na vinywaji?

Maana yake hakuna ufuatiliaji wa serikali ndiyo maana kimebaki kuwa chanzo cha mapato pekee na siyo ufuatiliaji wa kama huduma zinazotolewa zinakidhi matakwa ya kiafya kwa mujibu wa sheria.

Wasafiri ni watoto, vijana, umri wa kati na wazee ambao ni mchanganyiko wa wanaume na wanawake, wote wanatumia vyoo visivyoridhisha na ambao wako hatarini zaidi kupata maradhi ya njia ya haja ndogo ni wanawake na watoto.

Lazima hatua zichukuliwe tuone mabadiliko kuliko hali kuachwa ilivyo. Serikali isiishie kukusanya mapato pekee bali kujiridhisha na kusimamia usafi wa maeneo husika,kama inashindikana wachukue hatua kwa mujibu wa sheria.

Hoteli nyingi za Kanda ya Kaskazini mteja anaponunua chochote anapewa stakabadhi ya EFD lakini kwa hizi za Manispaa hii kwa uzoefu wangu wa kusafiri njia hiyo sijawahi kupewa stakabidhi maana yake hata Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) inapoteza mamilioni ya fedha ambazo zingeingia kwenye kapu la taifa na kutekeleza miradi ya maendeleo.

Kama hoteli za Kanda ya Kaskazini imewezekana kuweka mashine za EFD, basi hata Morogoro na mikoa mingine ambayo mamia ya wasafiri hutumia huduma, inawezekana kuweka stakabadhi hizo muhimu kwa maendeleo ya nchi yetu.

***Mungu ibariki Tanzania***











Hivi ndivyo shughuli ya Bahati Shabani ilivyofana, anawashukuru ndugu, jamaa na marafiki kwa kufanikisha vyema.

# MITINDO



# ‘TURTLENECK’

## Sweta linalokupa burudani

UNAPOTOKA maridadi kwenda ofisini au sehemu yoyote maalum ni jambo la kufurahisha na linalompatia mtu faraja na kujiamini.

Sweta lenye shingo ndefu maarufu kama ‘Turtleneck’ ni vazi linalong’arisha watu wa aina zote na ni moja ya nguo zinazoleta heshima na anasa kwa muhusika.

Hata hivyo, nguo hizi zinavaliwa katika nyakati maalum na hasa kwenye baridi kiasi kutokana na kitambaa chake kutengeneza joto.

Kwa ujumla sweta la aina hili huwatoa vilivyo wanawake na wanaume pale wanapolitumia kama vazi maalum la ofisi.

Sweta nyeusi ya turtleneck

Linapendeza zaidi kuvaliwa na mwanaume hasa kutokana na kuongeza mng’aro wa ngozi. Vizuri kama ukivaa na koti la rangi ya samawati au kahawia.

Kufanana kwa nguo za juu

Kama wewe ni mzuri katika kufananisha mavazi yako, unaweza kulinganisha baadhi ya nguo na sweta lako ili kukupatia matokeo mazuri.

‘Turtleneck’ kwa ujumla ni vazi linalovaliwa na wajanja wanaojua nini maana ya kutoka tofauti na kuonekana vizuri zaidi.



UREMBO

Na Mary Geofrey

# TUMIA KARANGA MBICHI Kutengeneza uso unaovutia



KARANGA ni aina ya nafaka ambazo mara nyingi zinatumika kama chakula, lakini zinaweza kukusaidia kwa sehemu kubwa kusafisha ngozi yako ya uso na mwili.

Karanga zinazohitajika ni zile mbichi. Kitu kinachohitajika ni kuchukua karanga ambazo hazijakaangwa kiasi kidogo kama kikombe kidogo cha chai.

Zianike juani kwa muda ili zimenyeke kwa urahisi. Saga kwa kutumia blenda au kitu chochote kitakachoweza kuzilainisha na kuwa unga laini.

Chukua unga wako wa karanga na uuchanganye na asali mbichi kiasi kidogo, kisha acha kwa muda wa dakika 10 ili vichanganyike.

Chukua mchanganyiko wako, kisha paka usoni hasa zile sehemu unazoziona kuwa na mikunjo zaidi.

Subiri kwa dakika kama 10, kisha osha uso wako na sabuni isiyo na kemikali baada ya hapo futa uso wako kwa kitambaa kisafi na kikavu.

Subiri tena kwa dakika tano halafu paka mafuta au losheni.

Unashauriwa kufanya hivi mara moja kwa wiki.

Kiasili njia hii imekuwa ikitumiwa na Wanyamwezi wa Tabora kama kipodozi kwa ajili ya mabinti wadogo pindi wanapokaribia kufanyiwa sherehe maalum.

Unaweza pia kusugua taratibu uso kwa kutumia mchanganyiko wako ili kuondoa takataka katika mwili wako ambapo baada ya kumaliza unaweza kujipodoa kwa kupaka aina nyingine za vipodozi.

Kwa kuwa hazina madhara, unaweza kufanya hivi kila siku na utafurahia matokeo yake.

MAPISHI

Na Mary Geofrey

# Makaroni ya nazi

MAKARONI ni chakula rahisi kupika na kinachowafaa watu wenye haraka kwa sababu hakihitaji muda mrefu kuiva.

**Mahitaji**

Makaroni pakiti moja, chumvi,siagi, vitunguu saumu vilivyopondwa,, tangawizi zilizopondwa, pilipili na tui la nazi.

Jinsi ya kupika

Tayarisha sufuria safi, weka maji ya kutosha. Ongeza chumvi kiasi na pilipili manga iliyosagwa.

Bandika jikoni na acha mpaka maji yachemke.

Weka makaroni kwenye maji yaliyochemka. Japokuwa maelekezo kwenye pakiti nyingi yanasema kuwa muda wa kupika ni dakika 10, hakikisha uivaji kwa kuyaonja. Baada ya kuiva, epua sufuria.

Tayarisha chujio na mimina makaroni ndani ya chujio ili kuchuja maji uliyochemshia makaroni.

Chukua maji ya vuguvugu miminia juu ya makaroni yakiwa bado ndani ya chujio.

Rejesha sufuria uliyochemshia makaroni jikoni huku ukiwa umepunguza sana moto.

Weka siagi ndani ya sufuria yako na iache iyeyuke vyema. Rejesha makaroni ndani ya sufuria yenye siagi. Waweza ongeza pilipili manga iliyosagwa kama ukipenda.

Koroga vizuri kwa dakika mbili ili mchanganyiko wa makaroni, pilipili manga na siagi ukolee barabara.

Makaroni yako yapo tayari kwa kuchanganywa na mboga.

Epua sufuria kisha pakua kwa kuku au chochote ukipendacho.



MAISHA NI NYUMBA

**Na Elizabeth Zaya**



# Jipange vizuri katika kusafisha nyumba yako

UCHAFU unachangia kwa kiwango kikubwa kuharibu nyumba hata kama ni nzuri na iliyojengwa katika uimara kiasi gani.

Mwingine anaweza kusema mbona kusafisha nyumba ni jambo linaloeleweka lakini ninachotaka kueleza ni namna gani unatakiwa kuweka kipaumbele na kujiwekea ratiba nzuri ya usafi wa nyumba yako yote.

Kumbuka kwamba nyumba ikisafishwa kwa umakini na ufasaha ni dawa inayojitosheleza katika kuimarisha na ikadumu zaidi. Kinyume chake, isiposafishwa vizuri ina uwezekano mkubwa wa kuharibika na kupoteza mvuto na uimara wake.

Jambo la msingi na la kuzingatia ni kwamba nyumba ina maeneo mengi na kila eneo linahitaji kusafishwa kwa umakini kwa ajili ya ustawi wake.

Ili ufanikiwe katika hilo ni lazima kujiwekea utaratibu mzuri wa kujipangia ratiba ya namna gani bora ya kufanya usafi katika kila eneo la nyumba yako.

Kwa mfano kama ni jikoni, chumbani, sebuleni, nje ya nyumba, stoo, vyooni na katika viunga vyote vya nyumba ni lazima kuhakikisha kwamba kote kunafanyiwa usafi wa uhakika kila mara.

Kwenye maeneo ya wazi yakiwamo yale yanayohitaji kufagiliwa, hakikisha unafanya hivyo. Kama umepanda maua, yahudumie nayo vizuri kwa kuyawekea mbolea na kuyamwagilia maji pamoja na kuyatengenezea mazingira ya kuendelea kustawi zaidi na yasigeuke kuwa uchafu kwenye nyumba.

Na baada ya kufanya usafi hakikisha unakagua kila eneo la nyumba ili kujiridhisha kama endapo kila mahali kumeguswa na usafi na kama kuna vitu ambavyo havihitajiki au havitumiki, viondoe.

Baada ya kusafisha, hakikisha kila kitu kwenye nyumba kimepangiliwa inavyostahili kuanzia jikoni, sebuleni, vyumba vya kulala, vyooni na hata nje ya nyumba kwenye bustani na sehemu nyinginezo.

Hakikisha yale maeneo yote ambayo yanahitaji kufanyiwa usafi kila siku inafanyika hivyo na usafi kwenye kila eneo la nyumba yako ndio utaiimarisha lakini endapo hakutakuwa na mpango mzuri wa kuisafisha utaiharibu.



## Namna ya kuchagua taulo



Namna ya kuchagua taulo

BAADA ya kuoga kila mmoja wetu anataka kujifuta mwenyewe ili kujikausha mwili kwa kitambaa kikubwa.

Hata hivyo, si wengi wanajua umuhimu wa kitambaa hiki ambacho maarufu kama taulo, katika utunzaji wa mwili hasa baada ya kuoga.

Unashauriwa kuwa na taulo bora ndivyo unaweza kujilinda mwili wako dhidi ya maradhi yanayotokana na maambukizi au fangasi.

**NAMNA YA KUCHAGUO TAULO**

1: Kabla ya kuamua na ununuzi, unahitaji kuelewa aina ya taulo unalohitaji, kama unajua ni muhimu kumshirikisha muuzaji.


2: Kitu muhimu ni ukubwa sahihi wa taulo. Hakikisha unanunua taulo lenye ukubwa unaoweza kulimudu wakati wa kujikausha maji, likiwa kubwa au dogo sana sio zuri.


3: Chagua taulo lenye kitambaa cha pamba asilimia 100 kwa sababu lina sifa ya kunyonya maji haraka.


4: Ulaini wa taulo ni jambo linalozingatiwa zaidi, kwani taulo likiwa laini litakufanya ujisikie vizuri wakati wa kujikausha kwa sababu halichubui au kuumiza ngozi.

# KATUNI







*KINYUNYIZO CHA LEO...




UTAJIRI WA MASIKINI 'SHIKAMOO'



Watu wakiwa juu ya daraja wakiwatazama wanakijiji wakitupa nyavu zao ili kuvua samaki katika ziwa linalofurika na kumwaga maji katika viunga vya Bangalore, nchini India juzi. PICHA: AFP

# Marekani yakubali kuanza mazungumzo na Russia

**WASHINGTON,** MAREKANI

MAWAZIRI wa Ulinzi wa Marekani na Russia, wamefanya mazungumzo kwa njia ya simu kwa mara ya kwanza kujadili vita vinavyoendelea nchini Ukraine.

Lloyd Austin wa Marekani na Sergei Shoigu kutoka Russia, walifanya mazungumzo hayo baada ya kufanya hivyo mwezi Mei, mwaka huu.

Waziri wa Ulinzi wa Marekani Austin, alisisitiza juu ya umuhimu wa kuendeleza mawasiliano wakati wa mazungumzo yake kwa njia ya simu na mwenzake Shoigu.

Wizara ya Ulinzi ya Russia imethibitisha mazungumzo hayo ikisema wakuu hao wamegusia suala la Ukraine bila ya kutoa maelezo zaidi.

Mara ya mwisho mawaziri hao kufanya mazungumzo ilikuwa ni Mei 13 wakati Austin alipoitolea mwito Russia kutekeleza usitishaji wa haraka wa mapigano nchini Ukraine.

Aidha, Austin alifanya mazungumzo tofauti na waziri mwenzake wa Ukraine, Oleksiy Reznikov,akisisitiza dhamira isiyoyumba ya Marekani ya kuunga mkono uwezo wa Ukraine wa kukabiliana na uvamizi.

Lakini Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani, Antony Blinken alisema kuwa haoni dhamira ya dhati kutoka kwa Russia juu ya mazungumzo mapana ya kumaliza vita vya Ukraine.

Blinken alisisitiza kwamba nchi yake itaendeleza mawasiliano na Russia, lakini juhudi pana za kidiplomasia zinategemea na utashi wa Rais Vladimir Putin, wa kukomesha uchokozi.

"Hatujaona ushahidi wa hilo kwa wakati huu. Kinyume chake, tunaona uchokozi wa Russia ukiongezeka maradufu," Blinken alieleza mkutano wa pamoja wa waandishi wa habari na waziri wa mambo ya nje wa Ufaransa Catherine Colonna.

Aliongeza kuwa tofauti ya kimsingi ni kwamba Waukraine wanapigania nchi yao, ardhi yao, mustakabali wao. Russia haipiganii hilo na ikiwa Rais Putin ataelewa hilo kwa haraka na kufikia hitimisho hilo, ndivyo wataweza kumaliza vita mapema.

Waziri huyo wa mambo ya nje wa Marekani, alikutana na waziri wa mambo ya nje wa Russia Sergei Lavrov mnamo mwezi Januari kuonya juu ya matokeo ya uvamizi, ambao Russia iliendelea nao mwezi mmoja baadaye.

Tangu wakati huo Blinken amekataa kuonana na Lavrov lakini alizungumza naye kwa njia ya simu mwezi Julai katika jitihada za kuwaachilia Wamarekani waliofungwa nchini humo.

Rais Joe Biden na Rais Vladmir Putin wote wameondoa matumaini ya mazungumzo ya mwezi ujao kando ya mkutano wa kilele wa kundi la nchi 20 zilizopiga hatua kiviwanda huko Bali Indonesia.

**UKRAINE YAZIDI KUSHAMBULIWA**

Taarifa mpya zinaeleza mashambulio makubwa yamefanyika jana asubuhi katika majimbo ya kati, magharibi na kusini mwa Ukraine.

Kulingana na taarifa hizo zinazotoka katika majimbo ya Ukraine, miundo mbinu ya umeme imeshambuliwa tena na jeshi la Russia.

Mshauri wa ofisi ya rais wa Ukraine, Aleksey Arestovich, alisema kuwa makombora matano yalifyatuliwa mjini Kiev, lakini yalidunguliwa na mfumo wa ulinzi wa anga. "Makombora yote matano yaliyopaa juu ya anga ya Kyiv yalidunguliwa na kuanguka ," alisema Arestovich

Polisi ya Ukraine ilionyesha picha za athari ambazo zilisababishwa na makombora yaliyoonekana ardhini baada ya kudunguliwa.

"Roketi ya wavamizi imedunguliwa kutoka juu ya moja ya wilaya za eneo la mji wa Kyiv. Hakuna waathiriwa na hakuna uharibifu, vifusi vilianguka katika msitu," alisema Andrei Nebitov, mkuu wa polisi wa Kyiv.

Aidha, makao makuu ya vikosi vya jeshi la Ukraine kusini, yaliripoti kwamba shambulio katika jimbo la Cherkasy lilitekelezwa kwa usaidizi wa ndege zisizokuwa na rubani za kamikaze.

"Moja ya miundo mbinu muhimu ya jimbo la Cherkasy ilipigwa," jeshi liliripoti.

Pia iliripotiwa kwamba safari za mbali mbali za treni zimechelewa kutokana na mashambulio ya usiku ambayo yaliharibu mfumo wa umeme.

**DW**

## Rais Xi Jingping apitishwa kuwania muhula wa tatu

**BEIJING,** CHINA

CHAMA cha Kikomunisti cha China, jana kimeridhia kimepitisha na kuimarisha nafasi ya Rais Xi Jingping katika uongozi wa nchi na kumuhakikishia kumpa muhula wa tatu madarakani.

Uongozi wa Xi Jingping haujawahi kushuhudiwa katika siasa za taifa hilo la pili kwa uchumi mkubwa duniani.

Hatua hiyo inamruhusu Xi kutangazwa rasmi kama rais wa China katika vikao vya serikali mnamo mwezi Machi. Katika kipindi cha wiki moja ya mkutano wa chama hicho tawala kilichohudhuriwa na wajumbe wapatao 2,300 mjini Beijing, yamefanyika mabadiliko makubwa ikiwa ni pamoja na waziri mkuu Li Keqiang kujitoa kwenye nafasi yake na kuruhusu Xi kuchagua wateule wengine.

Kabla ya kutamatishwa kwa mkutano huo wa chama wamechaguliwa pia wajumbe 200 wa kamati kuu ya chama

**DW**

## UN yaonya janga la njaa Somalia

**MOGADISHU,** SOMALIA

UMOJA wa Mataifa umesema msaada wa kimataifa wa chakula kwa Somalia ndiyo sababu pekee njaa inazuiwa katika taifa hilo linalozongwa na machafuko.

Hata hivyo shirika la Mpango wa Chakula Ulimwenguni la umoja huo (WFP), limetahadharisha ikiwa ulimwengu utasubiri hadi njaa kutangazwa kote ndipo uchukue hatua za dharura, utakuwa umechelewa.

Naibu mkurugenzi wa shirika hilo nchini Somalia, Laura Turner aliwaambia waandishi habari akiwa Mogadishu kuwa Somalia haijaondoka katika hali ya hatari, na kwamba wana wasiwasi kuhusu hali mbaya kuenea nchini kote.

Kulingana na Turner, viwango vya utapiamlo vinasikitisha huku vifo pia vikiongezeka na kusisitiza msaada wa haraka wa chakula unahitajika ili kunusuru mamilioni ya watu.

Somalia imekumbwa na miongo kadhaa ya vita vya wenyewe kwa wenyewe, ghasia za kisiasa na uasi wa makundi yenye itikadi kali na kusababisha watu kutumbukia katika mzozo wa chakula

**DW**

## MAKALA

# VIJANA NA UONGOZI WA NCHI YETU



Na Magabilo Masambu

NI ukweli kwamba ukitizama vijana wa zamani ambao leo ni wazee na vijana wa leo, kuna tofauti kubwa sana katika kufikiri kuhusu mambo ya msingi katika nchi, hasa kwenye eneo la uongozi. Sisi vijana wa leo tunafikiri zaidi kuhusu siasa za nchi kuliko uongozi wenyewe.

Pengine mtu anaweza kujiuliza unawezaje kufikiri juu ya siasa lakini usifikiri juu ya uongozi? Kama hautajua tofauti kati ya siasa na uongozi ni vigumu kutofautisha hizi dhana mbili. Leo tunazungumza siasa zaidi kuliko uongozi. Zamani walizungumzia zaidi uongozi kuliko siasa. Unaweza kumshawishi mtu kuingia katika siasa lakini huwezi kumshawishi kuingia kwenye uongozi.

Ikiwa utashawishiwa kuingia kwenye siasa wakati wewe si kiongozi, basi siasa inaweza kukupatia madaraka lakini ni vigumu kudumu katika uongozi kwa sababu, wewe si kiongozi. Kwa hiyo kuna uwezekano mkubwa kuwa na wanasiasa wengi ambao si viongozi. Yeyote anayetumia chama chake kubagua wengine, akitumia chama chake kuona anayo haki zaidi kuliko mwingine, huyo ni mwanasiasa asiyekuwa kiongozi.

Unaweza kujifunza siasa lakini huwezi kujifunza uongozi japo unaweza kujifunza taratibu za kuongoza. Ikiwa utajifunza taratibu za kuongoza ili hali wewe si kiongozi, tambua kuongoza kwako kutakuwa kugumu sana.

Katika taifa lolote vijana wanatakiwa kuandaliwa kwa ajili ya kuliendeleza taifa, si tu kupewa nafasi za kisiasa bali kuandaliwa katika fikra, wawe na uwezo wenyewe wa kujadili mambo ya kitaifa kwa utulivu bila mihemuko, bila kufundishwa kwamba piga yule au fanya hili kuhakikisha tunafanikiwa hapa. Cha msingi wapikwe kifikra na uwezo wa kujenga hoja sambamba na kujiamini kwamba wao wenyewe wanaweza kufanikiwa.

Siku hizi tumekuwa na msamiati mpya katika siasa za nchi yetu. Msamiati huo unaitwa "uchawa" na hili ni jambo hatari sana kwa vijana wa leo ambao tunategemea watakuwa viongozi wa kesho. Ikiwa tutawapa vijana nafasi za madaraka katika siasa kwa sababu ni chawa wetu, kama wanavyosema maana yake kuna hatari ya kupata viongozi vijana watakaokuwa na malengo ya kuwatumikia wale wanaowateua kuliko wananchi na taifa.

Hatari ya pili ni kwamba mnaweza kuwa na viongozi ambao hawawezi kujitegemea katika kufanya uamuzi. Kila jambo akifanya anafikiria yule aliyemteua atahisije ama atafurahi au atakasirika. Kwa hiyo itafika mahali tutapata viongozi goigoi na taifa halitasonga mbele.

Tukijenga utamaduni wa kuwapata viongozi hasa vijana kwa sababu wanatuposti kwenye mitandao ya kijamii, wanatusifu sana, wanatubebea mikoba, wanasema yale tunayoyapenda kusikia tu, basi kuna hatari ya kujenga taifa gumu sana huko mbeleni. Tuwapime vijana kwa fikra zao, maono yao hata kama wakati mwingine wanayoyasema hayatufurahishi sana, lakini kwa maslahi ya taifa hata kama vijana wa namna hiyo wakiwa ndani ya vyama vyetu tuwaandae zaidi kwa ajili ya kulijenga taifa letu kwa hapo baadaye.

Zamani watu walipitishwa kwenye vyuo vya uongozi wapate nafasi ya kujifunza siasa na uongozi. Chuo maarufu sana kilikuwa Kivukoni sina hakika kama mafunzo ya wakati ule yanatolewa mpaka sasa. Ni kweli kwamba pengine ni kwa sababu huko nyuma tulikuwa na mfumo wa chama kimoja, lakini hata sasa tunaweza kukubaliana mitaala yake iwe na mambo jumuishi ya kiinchi yasiwe ya kichama ili kila mtu kutoka chama chochote ajifunze misingi ya nchi yetu mambo ya vyama yasalie huko chamani.

Siku hizi imekuwa kawaida mtu akionekana tu anajua kuzungumza kwenye mkutano, anaitwa mwanasiasa, hivyo kufanya kila mtu au kila kijana kuwa mwanasiasa badala ya kiongozi. Watu wa aina hii wanapopata madaraka inakuwa changamoto sana. Tuwajenge vijana kwa ajili ya kutumika kwa pamoja kuijenga nchi na kuitetea mahala popote ndani au nje.

Utafutwe utaratibu pia wa kutufanya vijana tusione uongozi ni sehemu ya kujitajirisha, hivyo kufanya lolote ili tuzipate nafasi za madaraka. Ikiwezekana nafasi za kisiasa zipunguziwe mishahara ili kupata watu wenye moyo wa kuitumikia nchi kuliko kupata watu wanaotamani kuwa matajiri kupitia kwenye nafasi zao za uongozi.

Kuna watu wako nje ya madaraka wanaonekana wazuri na si wezi lakini kwa mfumo tulio nao leo, wakiyapata madaraka kuna uwezekano wa kufanya yale tunayoyaona kwa baadhi ya viongozi. Kwa hiyo mtazamo wa kuyapata madaraka usipobadilika tutaendelea kulia na wala rushwa, wezi, majambazi na kadhalika.

Vijana tubadilike tuamini tunaweza. Tujenge fikra za kuitumikia nchi kuliko kuwatumikia watu na haya masuala ya uchawa sasa yanakita mizizi kila mahali, si kwenye vyama vyetu tu bali sasa mpaka kazini. Mnafanya kazi kumbe kuna chawa katikati yenu. Haya mambo tusipoangalia tutavurugana huko kazini na kazi hazitafanyika. Jiamini mipango yako anaijua Mwenyezi Mungu.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**
**ARUSHA-TANZANIA**

## BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# Buriani Verckys, bendi, sax, nyimbo zako hazitosahaulika kwa Wabongo



Na Adam Fungamwango

NI Mtanzania gani mpenda muziki wa miaka ya 1970 hadi 1980 anazikumbuka bendi za Orchestra Veve, Kiam, Lipua Lipua, Les Kamale na Bella Bella.

Zilitingisha sana na nyimbo zake kuwa maarufu sana si hapa nchini tu, bali hata Afrika Mashariki. Zilimilikiwa kwa asilimia kadhaa na mwanamuziki maarufu sana, Kiamuangana Mateta, maarufu kama Verckys. Mwanamuziki huyo ambaye umaarufu wake, mbali na kumiliki bendi hizo ni mpiga ala ya upepo ambayo kitaalam au kimuziki inaitwa 'saxophone' alifariki dunia Oktoba 13, Kinshasa, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo.

Kwa mujibu wa mmoja wa wanamuziki aliyewahi kupiga naye muziki wakiwa nchini Congo, Tshimanga Kalala Assossa, mwanamuziki huyo alifariki dunia kwa ugonjwa wa kupooza.

Wanamuziki kadhaa nchini na duniani kote wametuma salamu za rambirambi kwa familia, ndugu jamaa na wanamuziki wote wa DRC kwa kumpoteza mwanamuziki huyo ambaye ni mtunzi, kiongozi wa bendi, mtayarishaji muziki na mfanyabiashara, akifariki dunia akiwa na umri wa miaka 78.

Mpiga saxophone wa zamani wa bendi za Jamhuri Jazz, Simba Wanyika na Mwenge Jazz, Luza Elius, akiongea kwa huzuni kutoka nchini Marekani, amesema kifo cha mwanamuziki huyo ni pigo kubwa si kwa mashabiki wa muziki tu na familia yake, bali hata kwake pia. Anasema ndiye aliyemfanya kupenda muziki na kukipenda chombo hicho hadi kupitia bendi zote hizo pamoja kuishi nchini Marekani kwa sasa.

Wako wanamuziki wengi nchini na nje ya nchi ambao walimfuata Verckys na kuiga upigaji wake na kufanikiwa kwa kiasi kikubwa. Wengine wako hai na wako waliotangulia mbele za haki.

Verckys alikuwa kiongozi na mmiliki wa bendi ya Orchestra Veve ambayo hapa nchini kwenye miaka ya 1970 ilitamba sana kwa vibao kama 'Baruti', 'Kalala', 'Lukani', "Mikolo Mileki Mingi', 'Muana Mburu', 'Nakomitunaka' na zingine nyingi. Bendi hii aliimiliki kwa asilimia 100 na Veve ilikuwa ni kifupi cha mwanzo wa jina lake,Verckys.

Bendi zingine alikuwa na hisa kutokana na kuwa yeye ndiye alikuwa akizifadhili vyombo na kutumia studio yake kuzirekodi.

Jamaa alijua mno kuzitafuta pesa kwani pamoja na kumiliki bendi, kupiga muziki, lakini alikuwa na studio nyumbani kwake na bendi zilizorekodi zilitumia lebo yake ya Edition Veve, lakini mwaka 1976 aliibadilisha jina na kuiita Zadis.

Kutokana na kuwa na hisa na bendi nyingi, mashabiki wake mbali na majina yake hayo, wakamuongezea na 'Wazolambongo', yaani 'mzoa pesa' akawa anaitwa Kiamuangana 'Wazolambogo' Mateta Verckys.

Bendi ya kwanza aliyokuwa na hisa nayo na kuifadhili ni Orchestra Bella Bella, ambayo kiongozi wake alikuwa ni Soki Vangu.

Ilirekodi kwenye studio yake nyimbo za 'Mbuta', 'Kamale', 'Sola' na nyingine nyingi ambazo nazo zilikuwa maarufu nchini watu wakinunua sana santuli zake.

Santuli zote hizo zilikuwa na chapa ya Edition Veve ambapo yeye mwenyewe alikuwa akirekodi kwenye studio yake na kuziuza zikampatia pesa nyingi yeye na bendi zenyewe.

Kulitokea mgogoro kwenye bendi ya Bella Bella, Soki Vangu aliondoka kwenda kuunda bendi nyingine, lakini akaondoka na jina. Akaunda Bella Bella nyingine. Waliobaki wakaachana na jina la Bella Bella na wakajiita Orchestra Lipua Lipua walilolichukua kwenye moja kati ya nyimbo zao wakati ikiitwa Bella Bella.

Lipua Lipua iliondokea kuwa maarufu mno ikitoa nyimbo zilizotamba Tanzania kama 'Mombasa', 'Mbondo', 'Mfueni','Kamale', 'Matoba' na zingine. Marehemu aliendelea kuwa mfadhili wa bendi zote hizo mbili.

Akakusanya wanamuziki wengine na kuunda bendi ya Orchestra Kiam ikiwa kifupi cha jina lake Kiamuangana. Nayo nyimbo zake zilipata mashabiki wengi nchini kama vile 'Moni Afinda', 'Kamiki', 'Mbale' na Memi. Assossa na Nyboma walijiondoa Lipua Lipua wakaenda kuunda bendi nyingine Les Kamale, Pepe Kalle yeye ambaye alikuwepo kwenye bendi hiyo tangu inaitwa Bella Bella, akaenda kuunda Empire Bakuba.

Les Kamale nayo ilichukua jina la wimbo wa Lipua Lipua 'Kamale', yenyewe ikatamba na nyimbo kama 'Andoya', Masua', 'Ngali', 'Aidjo', 'Abisina' na nyingine nyingi, na zote hizo zilikuwa chini ya lebo ya Edition Veve.

Alianza muziki kwenye bendi ndogo, lakini mwaka 1963 alijiunga na TP OK Jazz ya Franco, kabla ya kuunda bendi yake Veve mwaka 1969, na mwaka 1972

Alizaliwa kwenye familia ya kitajiri Mei 19, 1944 Congo ya Ubelgiji (sasa DRC) na baba yake alikuwa mfanyabiashara mkubwa jijini Leopoldville (sasa ni Kinshasa).

Alijifunza muziki kanisani, ikiwamo ujuzi wa kupuliza saxophone, chombo ambacho ndicho kilichompatia umaarufu mkubwa duniani.

Alimpenda sana mpiga saxophone maarufu sana wa Kimarekani wakati huo King Curtis, akawa anaiga upigaji wake hadi akaanza kujiita jina la mwanamuziki huyo.

Alijiita kimakosa kwani na matamshi ya Kifaransa jina 'Curtis' yeye alikuwa akisikia kama likitamkwa 'Verckys' na akawa anajiita hivyo.

# HADITHI

HAKUNA aliyeamini alichokisikia, wala aliyeamini macho yake kwa kile alichokiona. Awali kulikuwa na vigelegele, ngoma, bashasha na furaha tele kwa watu wote waliohudhuria harusi hiyo. Bwana harusi Jerry Mohamed aliliongoza kundi la ndugu, rafiki na jamaa kutoka Dar es Salaam kwenda Kibaha kwa Mathias mkoani Pwani kwa ajili ya kufunga ndoa na mwanamke Vayajo waliyekubaliana kuoana. Mabasi, magari, bajaj, bodaboda, vyote vilimiminika kwenda huko kila mmoja akiwa na furaha tele.

Kilichotokea ndicho kilicholeta mkasa mzima kwenye sakata hili la aina yake. Nini kimetokea? Kwa nini? Sababu ni nini? Na baada ya hapo nini kinaendelea? Kila nakala yako ya Nipashe itakupa majibu ya kisa hiki cha kushangaza.

# Harusi Imevunjika-2

**Na Adam Fungamwango**

**(0716 350534)**

"Jamani eee, samahanini kwanza, tumeona kwamba badala ya kuendelea na ratiba nyingine kwanza kipakuliwe chakula watu wale, maana wengine wametoka mbali Dar es Salaam tangu asubuhi hawajala, kwa hiyo msosi upakuliwe watu wale, na ratiba zingine zitaendalea kama zilivyopangwa."

Nia ya mzee yule ni kwamba watu wale chakula kilichopikwa kwanza, halafu kama baadaye itatangazwa habari hiyo mbaya, tayari kila mtu atakuwa ameshakula, tofauti na kile kilichopo sasa kama kitatangazwa, basi kuna watu hata kula hawatokumbuka tena kwa sababu halikuwa suala la kawaida.

Kwa sababu ni suala la chakula hakuna aliyehoji, na ni watu wachache sana waliofahamu tukio la kutoweka kwa bi harusi.

Sehemu kama hizo umbea haukosekani. Kuna baadhi wakaanza kuvujisha habari kabla hazijatamkwa rasmi. Wengi hawakuamini na ilionekana ni kama ni moja ya habari za mzaha tu ili kusukumizia chakula na vinywaji tu.

******************************

Tukio hilo lilipita kama ndoto ya jinamizi. Jerry alibaki anashinda ndani peke yake. Ilikuwa ni aibu kubwa. Aibu kwake, familia, ukoo na ndugu zake pia. Kuanzia Kibaha mpaka nyumbani kwao Tandika mtaa wa Berege, kila mtu alikuwa anaongea lake.

Kitu ambacho alikuwa anajiuliza ni kwa nini hakukataa kuolewa na yeye? Kwa nini alikubali kila kitu kifanyike? Alikubali sherehe, na alijiandaa kwa kila kitu hadi kupelekwa saluni kwa ajili ya kupambwa. Anavyofahamu yeye mwanamke ambaye hataki kuolewa angekataa tangu mwanzo. Na hata kama hatua kadhaa zingekuwa zimefanyika, lakini angeweza kukataa kwenda saluni.

"Ina maana hadi anakwenda kupambwa kwa ajili ya sherehe alikuwa bado anataka kuolewa, sasa imekuwaje atoroke dakika za mwisho?" Akajiuliza.

Kingine kilichomuumiza kichwa ni jinsi alivyotoroka. Hakuna yoyote aliyemuona. Alipotea kama mzuka tu. Haikumuingia akili kuwa bi harusi atoke ndani mle na aondoke mbali na eneo la nyumbani kwao bila kuonekana na mtu yoyote, hasa sehemu ile ambayo ilikuwa imeshona watu waliofurika kwa ajili ya harusi.




**Ndugu walianza kukaa vikundi vikundi, wengine waliziamini na wengine waliona ni kama wanadanganywa labda wanataka kufanyiwa 'sapraizi.'**

Alijiuliza kama alitoroka akiwa vile vile kama alivyo, alijibadilisha kwa kuvaa nguo nyingine, au alijibadilisha na kuvaa nguo ambazo hazikumtambulisha kama yeye ni nani.

Vyovyote vile ambavyo imetokea, bado haikuondoa kuwa lilikuwa tukio baya kuwahi kutokea kwenye maisha yake.

Anakumbuka jinsi yule mzee alivyowatangazia watu wale kwanza kabla ya kufunga ndoa, kumbe tayari walishagundua kuna tatizo na hata lilipotangazwa rasmi, tayari umma ulikuwa umeshatia kitu tumboni, vinginevyo baadhi ya watu wangeondoka bila kula na chakula cha sherehe kingemwagwa.

Anakumbuka pia kulikuwa na kutupiana maneno kati ya ndugu zake na ndugu za aliyetaka kumuoa, Vayajo.

"Nyinyi mnajua mlipompeleka mtoto wenu, haiwezekani yumo humo humo ndani na kuna mtu wa kumlinda halafu aondoke na awapotee hajulikani alipo. Mlitaka kula tu hiyo mahari. Au mmechukua mahari kwa wanaume wawili?" Anakumbuka dada yake Maonwa alivyocharuka siku hiyo.

"Hatukubali, mmetutia aibu kubwa, sasa kwa taarifa yenu hili halipiti hivi hivi, ni lazima tulipe, tutalipaje, sisi ndiyo tutajua, asanteni na kwaherini." Huyo alikuwa ni shangazi yake ambaye hakutaka kuondoka bila ya kupigwa mkwara wa aina yake.

Huko kwa bi harusi Kibaha, mambo yalikuwa mabaya zaidi nyumbani kwa bwana harusi. Wakati wanarejea, tayari baadhi ya watu walikuwa wameshapeleka ujumbe kuwa wanarejea mikono mitupu kwani bi harusi ametoroka.

Huko nako kulikuwa na sherehe ndogo nyumbani, lakini kubwa ilikuwa inataka kufanyika kwenye ukumbi mmoja ulio Tandika Mabatini. Ndugu walianza kukaa vikundi vikundi, wengine waliziamini na wengine waliona ni kama wanadanganywa labda wanataka kufanyiwa 'sapraizi.'

Msafara wa magari ulirejea kutoka Kibaha bila Vayajo. Kwa sababu Jerry alichukua likizo kazini kwake, ambayo ilikuwa ni maalum kwa ajili ya kujiandaa, kufunga ndoa na kwenda kula fungate, lakini sasa siku za likizo alizitumia kukaa ndani kwa mawazo, akifikiria vitu vingi vilivyomtia huzuni, akifarijiwa na baadhi ya ndugu na rafiki zake.

Siku ya pili tu baada ya tukio lile, baadhi ya ndugu hasa waliokuwa wanaishi mikoa ya mbali walianza kuondoka kwa sababu walichokifuata hakikuwepo.

Ulisikika mlio kwenye simu yake. Aliutambua kuwa ni wa meseji, lakini hakuutilia maanani. Siku hizi kwenye simu kuna meseji nyingi tu zinaingia zingine za kukutakia kila la heri tu. Ilipita karibuni dakika 10, hadi pale alipokuwa na hamu ya kutaka kushika simu yake, ndipo alipogundua kuna meseji ambayo hajaifungua.

"Pole kijana kwa yote yaliyotokea. Usihuzunike, wala kutukasirikia sisi wazazi wake. Hatujui ni kitu gani kimempata binti huyu. Na mpaka sasa hatujui alipo. Baadhi ya watu wameshauri tutoe ripoti polisi, lakini mimi nimewakataza, nimewambia upoteaji huu si ule wa mtu ambaye anakwenda kudhuriwa au kutekwa. Hapa kuna mambo ya ujana tu, wakipiga ripoti polisi halafu akapatikana anaweza kuwekwa ndani na hapo uhasama utakuwa mkubwa sana baina yetu. Huyu yupo na atarudi, lakini alichokifanya ni wewe pekee ndiyo utaamua. Kwa sababu hiyo tunakuomba siku ya Jumapili ijayo ufike Kibaha ili tuyajenge."

Aliisoma na kuirudia mara tatu. Ilikuwa ni simu ya babu yake Vayajo. Ni mzee mwenye akili nyingi, uwezo wa kutatua jambo na alikuwa anaelewana naye sana. Kifupi alikuwa ni rafiki yake mno, kuliko hata wazazi wa msichana huyo.

Jerry alifikiri kama aende au asiende. Aibu aliyoipata siku ile kila mtu anamuangalia yeye, leo arudi tena Kibaha 'ajichoreshe' "Hapana" alijiambia.

Akakumbuka pia aliapa wakati anarejea kuwa hatorudi tena kule, kwa sababu atakapokuwa anaona madhari ya eneo lile la Kibaha atakuwa anamkumbuka Vayajo na madhila yote aliyomfanyia. Dakika moja baadaye akakumbuka kitu.

Akakumbuka mara ya kwanza alipopelekwa Kibaha na Vayajo, siku za mwanzo tu za penzi lao baada ya kukutana maeneo ya Chang'ombe Dar es Salaam na kutokea kupendana alimwambia kuwa huko anaishi kwa dada yake, lakini kwao hasa ni Kibaha.

Kutokana na kuwa kwenye lindi la mahaba ya mwanzoni, Vayajo aliamua kumpeleka nyumbani kwao. Akamhakikishia kuwa hakuna kitu chochote kitakachomtokea, japo Jerry alimwambia haitokuwa vema kwenda nyumbani kwao wakati wazazi hawamfahamu na hajatambulishwa rasmi.

**ITAENDELEA JUMAPILI**

HABARI BURUDANI



# UTANASHATI JUX NOMA

MSANII wa muziki wa kimahaba, Juma Jux, inaelezwa anaongoza kwa kuwa na mwonekano mzuri kuliko wanamuziki wote nchini.

Kulingana na tathimini ya mkongwe wa hiphop, Soggy Doggy Anter, amesema yeye hata akilala anaposhtuliwa kumtaja msanii gani msafi Tanzania, jibu la haraka litakuwa ni Jux.

"Mimi niliwahi kuwa naye kule Mwanza, nilishuhudia jinsi Jux alivyokuwa msafi, alikuwa akioga mara kwa mara na siku zote huwa ananukia," amesema Soggy Doggy.

# TUNDAMAN AJIWEKA REHANI



MSANII wa BongoFleva na shabiki wa Klabu ya Simba, Tundaman ameapa kutojishirikisha kuimba nyimbo zinazoisifu timu hiyo kama watafungwa na watani wao Yanga.

Akizungumza na EATV, Tundaman amesema kujiamini kwake huko kunatokana na timu yake kuwa na wachezaji wazuri zaidi ya wapinzani wao.

"Tuna wachezaji wazuri zaidi, japokuwa tulikuwa na changamoto ya makocha, Mgunda ameweza kuleta matumaini mapya ya kupambana. Safari hii tukifungwa tena na watani siimbi tena nyimbo za Simba," amesema Tundaman

## ZISIKUPITE

### RONALDO SAFARI IMEIVA
KLABU ya Manchester United inatafakari kuhusu kumwachia, Cristiano Ronaldo kwenye uhamisho wa bure baada ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 37, raia wa Ureno kutemwa kwa kukataa kuingia kama mchezaji mbadala katika mechi dhidi ya Tottenham siku ya Jumatano. ***(The Sun)***

### FELIX KUMRITHI RONALDO
HUENDA Manchester United wakamwania mchezaji wa kiungo cha mbele wa Atletico Madrid na raia wa Ureno, Joao Felix, mwenye umri wa miaka 22, kama mchezaji atakayeichukua nafasi ya Cristiano Ronaldo katika dirisha dogo la Januari. ***(Deportes Cuatro)***

### AMORIM ANUKIA VILLA
KOCHA wa Sporting Lisbon, Ruben Amorim yupo kwenye orodha ya Aston Villa kwa ajili ya kurithi mikoba ya Steven Gerrard, lakini bosi wa zamani wa Tottenham, Mauricio Pochettino hana nia na fursa hiyo. ***(The Athletic)***

### TUCHEL AIKATAA VILLA
ALIYEKUWA Kocha wa Chelsea, Thomas Tuchel pia hana nia ya kuichukua nafasi hiyo ya ukocha katika kikosi cha Aston Villa. ***(Telegraph)***

### NDICKA AKARIBIA ARSENAL
KLABU ya Arsenal inamwania mlinzi mwenye umri wa miaka 23 wa Eintracht Frankfurt, Evan Ndicka. ***(Evening Standard)***

### HAALAND MKATABA MPYA
WAKALA wa mshambuliaji wa Manchester City, Erling Haaland, mwenye umri wa miaka 22, amekaribisha uwezekano wa raia huyo wa Norway kutia saini mkataba mpya na klabu hiyo. ***(90min)***

### JONG ANUKIA ENGLAND
CHELSEA, Liverpool na Manchester United zipo tayari kumwania mchezaji wa kiungo cha kati wa Uholanzi, Frenkie de Jong ifikapo Januari iwapo mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25 ataamua kuondoka Barcelona. ***(ESPN)***

### ZAHA KUONDOKA PALACE
NYOTA wa Timu ya Taifa ya Ivory Coast, Wilfried Zaha, mwenye umri wa miaka 29, huenda akakataa mazungumzo ya mkataba mpya na Crystal Palace wakati akitafuta uhamisho wa bure kuelekea katika klabu iliyo katika nafasi sita za juu kwenye ligi msimu ujao wa joto. ***(The Five Podcast, via Mail)***

### MOUKOKO SOKONI ULAYA
LIVERPOOL, Paris St-Germain, Real Madrid na Barcelona zinamwangalia mchezaji wa Borussia Dortmund mwenye umri wa miaka 17 ambaye ni raia wa Ujerumani anayecheza kwenye timu ya vijana ya umri chini ya miaka 21 -Youssoufa Moukoko. ***(Football Insider)***

### NEVES AITAMANI BARCA
BARCELONA imepewa fursa ya kumsajili mchezaji wa kiungo cha kati wa Wolves Mreno, Ruben Neves, mwenye umri wa miaka 25, anayekiri kwamba anavutiwa na uwezekano wa kuichezea timu hiyo kubwa ya Hispania. ***(Mundo Deportivo)***

### MC KENNIE KUTUA JUVENTUS
KLABU ya Tottenham Hotspur inafikiria kumwania raia wa Marekani, Weston McKennie wa Juventus ifikapo Januari. ***(Calciomercato)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# HAALAND ATARAJIWA KUWA MCHEZAJI GHALI

●●●Wakala wake asema thamani ya mshambuliaji huyo kwa sasa imefikia pauni...

**MANCHESTER, England**

ERLING Haaland anaweza kuwa mchezaji wa kwanza katika soka la dunia kufanya uhamisho wenye thamani ya pauni bilioni moja, kwa mujibu wa wakala wake, Rafaela Pimenta.

Haaland aliondoka Borussia Dortmund na kujiunga na Manchester City kwa ada ya pauni milioni 51.2 Mei, mwaka huu na mshambuliaji huyo tayari ameanza maisha mazuri kwenye Ligi Kuu England.

Raia huyo wa Norway amekuwa mchezaji wa kwanza kufunga mabao tisa katika mechi zake tano za kwanza za ligi hiyo maarufu na tayari amefunga hat-trick tatu kwenye mashindano hayo.

Haaland amefunga mabao 15 katika mechi 10 za Ligi Kuu England akiwa na City, na Pimenta, anaamini anaweza kuweka historia kwa kuhama kwake tena.

Alipoulizwa kuweka bei kwa Haaland na Sky Sport Italia, Pimenta alisema: “Bilioni moja, ndivyo ninavyofikiria.

“Ukiweka pamoja thamani yake ya soka, thamani ya taswira yake, thamani yake ya udhamini, ni bilioni moja, bila shaka.

“Pia ni jambo la kawaida kumlinganisha Erling na (Kylian) Mbappe, kwa hivyo una wazo kidogo la soko. Nafikiri Erling atakuwa mchezaji wa kwanza kufikia uhamisho wa takribani bilioni moja.”

Kiwango cha ajabu cha Haaland kimeendana na uvumi unaomhusisha na Real Madrid, lakini Pimenta atakuwa tayari kujadili mkataba mpya na City badala ya kuanzisha uhamisho.

Alipoulizwa kama Haaland anaweza kuwa tayari kupata mkataba mpya, alisema: “Natumai hivyo! Kama wanataka kulijadili leo, nitafurahi.”

SportPesa | LIVE IN PLA

MECHI KALI
YOUNG AFRICANS
VERSUS
SIMBA
1 | 2.55
X | 2.75
2 | 2.90

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# CONTE AHOFIA KUMKOSA KULUSEVSKI KATIKA EPL



**LONDON, England**

ANTONIO Conte ana wasiwasi, Dejan Kulusevski huenda asiichezee Tottenham kabla ya Kombe la Dunia baada ya winga huyo kupata shida katika kupona jeraha la misuli ya paja.

Kulusevski hajashiriki katika kikosi cha Spurs tangu mwezi uliopita walipofungwa mabao 6-2 na Leicester City, baada ya kupata jeraha hilo akiwa kwenye majukumu ya kimataifa.

Ingawa awali uchezaji wa Richarlison uliiruhusu Spurs kukabiliana na kukosekana kwa Kulusevski, mshambuliaji huyo wa Brazil alichechemea kutokana na ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya klabu yake ya zamani ya Everton wiki iliyopita, na hivyo kumwacha Conte akikosa chaguo la mshambuliaji.

Akizungumza kabla ya pambano la leo dhidi ya Newcastle United, Conte alisema kuhusu Kulusevski: "Nadhani tunapaswa kusubiri muda kidogo kumwona pamoja nasi, ni vivyo hivyo kwa Richarlison.

"Kwa hakika, hali ya aina hii huleta ugumu mkubwa. Ni kawaida. Kwangu mimi, pia vidole vilivuka kwa sababu kwa sasa tuna Harry (Kane) na Sonny (Son Heung-min) katika afya njema.

"Unapoenda kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya, haswa ikiwa unacheza Ligi Kuu, lazima ujue utakuwa na msimu mgumu wa majeruhi, kwa michezo mikubwa, kwa wachezaji wanaochoka."

# James nje Kombe la Dunia

**LONDON, England**

REECE James alikiri ameambiwa na daktari wa upasuaji anaweza kuwa nje kwa miezi miwili kutokana na jeraha la goti alilopata kwenye mchezo dhidi ya AC Milan.

James alikuwa kwenye nafasi ya kujumuishwa katika kikosi cha England cha Gareth Southgate kitakachoshiriki Kombe la Dunia nchini Qatar mwezi ujao lakini majeraha ya goti lake yanaweza kukatiza azma yake.

Beki huyo wa Chelsea mwenye umri wa miaka 22 alipewa nafasi ya kuanza katika mechi mbili za mwisho za England na kocha Southgate katika hali ya kuonyesha imani yake kabla ya michuano hiyo, na sasa anaonekana kukosa



nafasi kabisa.

"Wiki iliyopita niliingia kwa ajili ya kukabiliana na AC Milan nilipojeruhiwa," alisema James aliwaambia mashabiki kwenye video ya YouTube.

"Sikufikiri ilikuwa mbaya sana baada ya mchezo, nilikaa siku ya ziada huko Milan na nilifikiri labda ilikuwa ni kusumbuka kidogo. Nafikiri siku moja au mbili baadaye nilimwona daktari wa upasuaji. Aliniambia ningeenda nje kwa takriban miezi miwili."

James amekuwa katika kiwango kizuri mwanzoni mwa kampeni za Chelsea za 2022-23, akiwa na mabao mawili na asisti mbili katika mechi 11 katika michuano yote. Lakini sio tu kwenda mbele ambapo mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22 amevutia, kwani pia amefunga mabao manne safi katika kipindi hicho.

HABARI MICHEZO

CHEZA USHINDE KASINO

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SPORTPESA APP

PAKUA APP YETU, BET LEO UWE MILIONEA

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAPILI - 23/10/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 4799 | Dynamo Kiev vs Vorskla Poltava | 1.36 | 4.38 | 7.21 |
| 13:15 | 2609 | SBV Excelsior vs AZ Alkmaar | 6.95 | 4.97 | 1.36 |
| 13:30 | 1591 | Udinese vs Torino | 1.96 | 3.32 | 3.72 |
| 14:00 | 2777 | Angers vs Rennes | 3.99 | 3.79 | 1.78 |
| 15:00 | 2831 | Espanyol vs Elche | 1.72 | 3.66 | 4.61 |
| 15:30 | 1786 | Cambuur vs Twente | 4.16 | 3.76 | 1.74 |
| 15:30 | 4541 | Groningen vs PSV Eindhoven | 7.75 | 5.16 | 1.32 |
| 15:30 | 5279 | NEC Nijmegen vs GO Ahead Eagles | 1.92 | 3.41 | 3.76 |
| 16:00 | 1107 | Wolverhampton vs Leicester | 2.23 | 3.27 | 3.07 |
| 16:00 | 1930 | Toulouse vs Strasbourg | 2.19 | 3.44 | 3.04 |
| 16:00 | 2116 | Bologna vs Lecce | 2.13 | 3.11 | 3.45 |
| 16:00 | 2242 | Reims vs AJ Auxerre | 1.77 | 3.63 | 4.27 |
| 16:00 | 3814 | Southampton vs Arsenal | 4.91 | 3.96 | 1.60 |
| 16:00 | 3942 | Leeds vs Fulham | 2.01 | 3.46 | 3.41 |
| 16:00 | 4207 | Troyes vs Lorient | 2.32 | 3.38 | 2.88 |
| 16:00 | 5176 | Aston Villa vs Brentford | 2.07 | 3.37 | 3.32 |
| 16:00 | 5340 | Clermont Foot vs Brest | 2.33 | 3.28 | 2.93 |
| 16:30 | 1564 | Spartak Moscow vs FK Khimki | 1.21 | 6.12 | 10.85 |
| 16:30 | 3977 | VfL Bochum vs Union Berlin | 3.97 | 3.38 | 1.88 |
| 17:00 | 1450 | Adana Demirspor vs Konyaspor | 2.16 | 3.39 | 3.14 |
| 17:00 | 1659 | Young Africans vs Simba | 2.55 | 2.75 | 2.90 |
| 17:00 | 2613 | Karmiotissa vs Akritas Chlorakas | 2.09 | 3.30 | 3.45 |
| 17:00 | 5765 | KAA Gent vs RFC Seraing | 1.36 | 4.97 | 7.16 |
| 17:15 | 5510 | Betis vs Atletico Madrid | 3.16 | 3.21 | 2.27 |
| 17:30 | 1460 | Maritimo vs FC Arouca | 2.55 | 3.20 | 2.70 |
| 17:30 | 3907 | FC Zurich vs Grasshoppers | 1.74 | 3.83 | 4.18 |
| 17:45 | 5485 | Utrecht vs Sparta Rotterdam | 1.74 | 3.61 | 4.36 |
| 18:00 | 2807 | Bodo Glimt vs Kristiansund | 1.16 | 7.56 | 11.94 |
| 18:05 | 4009 | Nice vs Nantes | 1.82 | 3.52 | 4.17 |
| 18:30 | 1791 | Tottenham vs Newcastle | 2.05 | 3.43 | 3.33 |
| 18:30 | 3664 | Hertha BSC vs Schalke 04 | 1.71 | 3.77 | 4.37 |
| 18:30 | 4373 | Cracovia vs Lech Poznan | 2.97 | 3.21 | 2.22 |
| 18:30 | 5885 | Dunajska Streda vs Sport Podbrezova | 1.59 | 3.99 | 4.57 |
| 19:00 | 2865 | Aarhus vs Brondby | 2.39 | 3.43 | 2.74 |
| 19:00 | 3221 | Akhmat Grozny vs Torpedo Moscow | 1.46 | 4.26 | 6.34 |
| 19:00 | 4282 | Aris Limassol vs EN Paralimni | 1.40 | 4.60 | 7.20 |
| 19:00 | 4944 | Samsunspor vs Boluspor | 1.79 | 3.51 | 3.90 |
| 19:00 | 5713 | Atalanta vs Lazio | 1.93 | 3.56 | 3.56 |
| 19:30 | 2217 | Girona vs Osasuna | 2.55 | 3.11 | 2.80 |
| 19:30 | 3146 | PAOK vs Asteras Tripolis | 1.48 | 3.88 | 6.97 |
| 19:30 | 4793 | Villarreal vs Almeria | 1.37 | 4.80 | 7.60 |
| 19:30 | 5229 | Standard Liege vs Anderlecht | 2.98 | 3.43 | 2.23 |
| 19:30 | 5918 | Panathinaikos vs Aris Salonica | 1.82 | 3.19 | 4.69 |
| 20:00 | 1136 | Molde vs Rosenborg | 1.90 | 3.69 | 3.59 |
| 20:00 | 1964 | Galatasaray vs Alanyaspor | 1.57 | 4.08 | 5.17 |
| 21:00 | 2290 | FC Volendam vs Heerenveen | 3.17 | 3.47 | 2.10 |
| 21:00 | 3172 | Universitatea Cluj vs CFR Cluj | 3.61 | 3.07 | 2.10 |
| 21:45 | 3350 | Lille vs Monaco | 2.40 | 3.49 | 2.69 |
| 21:45 | 5337 | Roma vs Napoli | 2.81 | 3.41 | 2.32 |
| 22:00 | 1883 | Barcelona vs Athletic Bilbao | 1.61 | 4.08 | 4.94 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# SIMBA QUEENS YAIFUNGA MDOMO YANGA PRINCESS

**Saada Akida na Shufaa Lyimo**

TIMU ya Simba Queens imefanikiwa kulipiza kisasi kwa watani zao, Yanga Princess baada ya kuibuka na ushindi wa mabao 2-0 katika mechi maalumu ya Tamasha la Michezo la Wanawake (Tanzanite Festival 2022) iliyochezwa kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam jana.

Mabao ya Simba katika mchezo huo yalifungwa na Oppa Clement dakika ya 61 na lingine lilipachikwa na Mkenya, Jentrix Shikangwa dakika ya 87 na kufanya wapate zawadi ya Sh. milioni tatu wakati wapinzani wao Yanga Princess waliambulia Sh. milioni 1.5.

Katika mechi ya mapema asubuhi, Baobab Queens waliwatamba majirani zao, Fountain Gate Princess baada ya kuibuka na ushindi wa penalti 9-8 baada ya sare ya bao 1-1 katika dakika 90 za kawaida.

Baobab Queens pia walizawadiwa Sh. milioni tatu na wapinzani wao walipata Sh. milioni 1.5.

Katika upande wa netiboli, Tanzania iliibuka kidedea kwa kuifunga Uganda magoli 45-44 huku ngumi ilitawaliwa na mabondia kutoka Zambia, ambapo Meredith Ngona alimchapa Mtanzania Mariam Richard uzito wa kilogramu 48 na Katherine Mwape akimdunda Shakira Abdallah.

Akifunga tamasha hilo, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Tulia Ackson, alilitaka Baraza la Michezo la Taifa (BMT) kuendelea kufufua michezo iliyopotea na kuibua vipaji vya wachezaji chipukizi kutoka kwenye vituo mbalimbali vya michezo hapa nchini.

Alisema aliitaka BMT kuongeza hamasa ya kuitangaza michezo ya wanawake ili iongezeke kam ilivyo kwa wanaume.

"Niwapongeza Wizara ya Utamaduni Sanaa na Michezo kwa kushirikiana na BMT kwa kuandaa tamasha hili ambalo ni kuunga mkono juhudi za Rais wetu, Samia Suluhu Hassan, kwa kuwekeza katika michezo ya wanawake kwa kuwa na tamasha hili ," alisema kiongozi huyo.

Pia aliipongeza wizara inayoshughulika na michezo kwa kuandaa tamasha hilo lililoshirikisha michezo mbalimbali ikiwamo mchezo wa rede ambao ulipotea. Naye msanii wa bongo fleva nchini, Said Juma maarufu Chege, alifanikiwa kuwapagaisha mashabiki waliofika katika kilele cha tamasha hilo ambalo mwaka huu linafanyika kwa mara ya pili.



Wachezaji wa Simba Queens wakishangilia baada ya kukabidhiwa kikombe kufuatia ushindi wa mabao 2-0 walioupata kwa kuwafunga Yanga Princess katika mechi maalumu ya Tamasha la Wanawake iliyochezwa kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam jana. **PICHA: SAADA AKIDA**

## Serengeti Girls

INATOKA UK. 24

iliyochezwa Oktoba 15, mwaka huu ilipata ushindi wa mabao 2-1 na kuwaacha vigogo hao wakiwa hawaamini kilichotokea. Ushindi huo uliongeza ari ya wachezaji wa Serengeti Girls kuelekea mchezo wa mwisho dhidi ya Canada ambao ulimalizika kwa sare ya bao 1-1, matokeo hayo yakiwa bora kwa Watanzania lakini yakiwaliza Canada ambayo ilihitaji ushindi tu ili isonge mbele.

Nigeria ilifanikiwa kutinga hatua ya nusu fainali kwa penalti 4-3 dhidi ya Marekani baada ya dakika 90 kumalizika kwa sare ya bao 1-1.

## Simba SC, Yanga hesabu uwanjani

INATOKA UK. 24

wao," alisema Mauya.

Kocha Mkuu wa Simba, Juma Mgunda, alisema kikosi chake kiko tayari kupambana, na anajua mechi itakuwa na ushindani na wao kama Wekundu wa Msimbazi wanatarajia kushinda ili kujiweka katika mazingira mazuri kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

"Tutamkosa Shomari Kapombe na Jimmyson Mwanuke pekee ambao ni wagonjwa, lakini wengine wote wapo sawa, mpira hautembei ila boli litapigwa, kikubwa ni kuomba kila mmoja aamke salama," alisema Mgunda.

Nahodha Msaidizi wa Simba, Mohammed Hussein 'Zimbwe Jr', alisema wanatambua kama utakuwa mchezo mgumu na wanawaheshimu Yanga lakini wamepania kufanya vizuri.

"Hatuangalii ubora wa mchezaji mmoja mmoja, tumejiandaa kuwazuia wapinzani wetu, naamini kwa umoja tulionao tutaondoka uwanjani na pointi tatu muhimu," alisema nyota huyo. Simba inaongoza msimamo wa ligi baada ya kucheza mechi tano, imevuna pointi 13 sawa na Yanga inayoshika nafasi ya pili zikitofautiana mabao ya kufunga na kufungwa.

Mashindano ya ZFF, mchezo huo umesog

# Michezo

Jumapili Oktoba 23, 2022

Nipashe




**Haaland atarajiwa kuwa mchezaji ghali**

UKURASA 21




Juma Mgunda- Simba




Nasreddine Nabi- Yanga

# Simba SC, Yanga hesabu uwanjani

## Nabi ajipanga kufuta machungu ya CAF, Mgunda akisema boli litapigwa...

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

MUDA umewadia wa mafahari wa soka na watani wa jadi nchini, Simba na Yanga kukutana katika mechi ya kwanza ya Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu itakayochezwa leo kuanzia saa 11:00 jioni kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Kwa sasa dabi hiyo si tu inafuatiliwa na mashabiki wa soka nchini, imevuka mipaka na kutazamwa pia na wadau kutoka mataifa mbalimbali na kuifanya iendelee kuwa na mvuto.

Licha ya mechi hizi kuzungukwa na tambo, majigambo na maneno mengi, lakini dabi ya leo imekuja wakati timu hizo zikiwa zimetoka kwenye joto la mashindano ya kimataifa, Ligi ya Mabingwa Afrika ambapo Simba imetinga hatua ya makundi huku Yanga ikitolewa.

Kutolewa kwa Yanga katika michuano hiyo kunaonekana kama kuwanyong'onyesha mashabiki wake na wanatarajia kutumia mechi hiyo kuwaomba msamaha na kuwafuta machozi, kama Ofisa Habari wake, Ali Kamwe, alivyosema huku Simba ikitaka kudhihirisha mafanikio yake ya kutinga hatua ya makundi Ligi ya Mabingwa Afrika kutawaongezea nguvu na haikuwa kwa kubahatisha.

Simba wanadai wanakwenda kuivaa Yanga hali ya kuwa hawajali chochote kwa sababu wao akili na nguvu zao zinaelekezwa kushindana na vigogo wa Afrika akiwamo Al Ahly na si watani zao, ambao leo ni wenyeji wa mchezo huo.

Mara ya mwisho Simba kupata ushindi dhidi ya Yanga kwenye mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara ilikuwa ni Februari 16, mwaka 2019 kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, kwa bao 1-0 lililowekwa wavuni na, Meddie Kagere ambaye kwa sasa anaichezea Singida Big Stars.

Baada ya hapo timu hizo zimecheza mechi tano za ligi hiyo, Yanga ikipata ushindi mara mbili na sare tatu.

Mara zote hizo tatu Yanga ilikuwa ikipata ushindi wa bao 1-0, Machi 8, mwaka 2020 ilishinda kwa lililofungwa na Benard Morrison ambaye kwa sasa amerejea kwenye timu hiyo, na Julai 3, mwaka jana kwa bao la Zawadi Mauya, sare ambazo timu hizo zilitoka ni ya mabao 2-2 Januari 4, 2020 ya Mapinduzi Balama na Mohamed Banka kwa Yanga, huku Kagere na Deo Kanda waliifungia Simba.

Novemba 7, 2020 zilitoka sare ya bao 1-1 ya Michael Sarpong kwa Yanga na Joash Onyango upande wa Simba, na mara ya mwisho Desemba 11, 2021 zilitoka suluhu.

Hata hivyo, timu hizo zilipopambana kwenye mechi ambazo si za Ligi Kuu, Simba iliifunga Yanga bao 1-0 kwenye fainali ya Kombe la FA kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika, Kigoma Julai 25, 2021 lililofungwa na Thadeo Lwanga ambaye ameshaondoka kwenye timu hiyo, huku Yanga ikiifunga Simba mabao 2-1 Agosti 13 mwaka huu, magoli yaliyofungwa na wachezaji ambao bado wamo kwenye timu hizo na wanatarajia kucheza, Fiston Mayele akifunga kwa upande wa Yanga na Pape Sakho, akiifungia Simba.

Akizungumza na gazeti hili kuelekea mechi hiyo, Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, alisema wamesahau matokeo yote ambayo wamewahi kuyapata katika michezo yote iliyopita na wamejiandaa kufanya vizuri katika mchezo wa leo.

Nabi alisema wataingia katika mechi hiyo wakicheza kwa tahadhari kwa sababu Simba itakuwa na presha ya kulipiza kisasi na kuendeleza matokeo chanya ambayo imepata tangu kuanza kwa msimu huu.

"Nimewaandaa wachezaji wangu kwa ajili ya kufanya vizuri katika mchezo huu, nimewaongoza Yanga katika dabi nyingi, hivyo nina uzoefu tayari, naomba mashabiki watarajie matokeo mazuri," alisema Nabi.

Kocha huyo alisema wachezaji wote wapo vizuri na kumtaja nyota ambaye atakosa mchezo huo ni Benard Morrison ambaye anatumikia adhabu.

Kiungo, Zawadi Mauya, akizungumza kwa niaba ya wachezaji wa Yanga, aliwataka mashabiki na wanachama wa timu hiyo kutokuwa na wasiwasi na hofu ya aina yoyote.

Mauya alisema wachezaji wenzake wamemtaka aseme wao wako tayari kwa mechi hiyo na wanaamini watapata matokeo mazuri mbele ya watani zao.

"Tutafuata yale yote tuliyoelekezwa na kocha wetu, tunaimani tutafanya vizuri licha ya mchezo huo kutarajiwa kuwa mgumu kutokana na ubora ambao wanao wapinzani

INAENDELEA UK . 23

## Serengeti Girls yamaliza kibarua

**Na Adam Fungamwango**

SAFARI ya Timu ya Soka ya Taifa ya Wasichana wa umri chini ya miaka 17 (Serengeti Girls) katika Fainali za Kombe la Dunia imemalizika baada ya kukubali kichapo cha mabao 3-0 kutoka kwa Colombia katika mechi ya hatua ya robo fainali iliyochezwa kwenye Uwanja wa Pandit Jawaharlal Nehru, Goa nchini India, jana.

Mabao yote ya Colombia katika mechi hiyo yalifungwa katika kipindi cha kwanza.

Matumaini ya Watanzania kuweka historia nyingine kwenye soka la wanawake yalianza kufifia dakika ya tatu, pale Colombia ilipopata bao la kwanza kupitia kwa straika wake hatari, Linda Caicedo aliyepokea mpira kutoka kwa Gabriella Rodriguez.

Caicedo alifungua ukurasa huo wa magoli baada ya hesabu za golikipa wa Serengeti Girls, Zulfa Makau kupotea akiwa kwenye jitihada za kutaka kuuwahi mpira, lakini kasi yake ikawa ndogo kuliko mfungaji ambaye alidokoa kidogo na kufunga bao hilo.

Dakika ya 17, timu hiyo kutoka Bara la Amerika Kusini iliandika bao la pili lililofungwa kwa kichwa na Yesica Munoz aliyeruka juu mbele ya mabeki watatu wa Serengeti Girls, akiunganisha krosi kutoka kwa beki wa kushoto, Christina Motta.

Makau alimwangusha mchezaji hatari Yesica, dakika ya 33 na mwamuzi akaamuru penalti, lakini wakati huo huo, Kocha Mkuu wa Serengeti Girls, Bakari Shime, akalazimika kumtoa kipa huyo aliyeonekana hakuwa katika kiwango chake ikichozoeleka na nafasi yake ikachukuliwa na Husna Mtunda, ambaye ilionekana pia kama angeweza kwenda kuokoa tuta hilo.

Hata hivyo Mtunda hakufanikiwa, kwani Gabriella aliukwamisha wavuni kulia kwa kipa huyo. Mechi hiyo kwa kipindi kirefu cha kwanza ilichezwa huku mvua kubwa ikinyesha.

Serengeti Girls imetolewa katika michuano hiyo ikiwa imeweka heshima kubwa, ilisifiwa na vyombo mbalimbali vya habari vya nchi zilizoshiriki fainali hizo kutokana na uwezo mkubwa na vipaji vya wachezaji wake.

Kwa mara ya kwanza Serengeti Girls ilishiriki fainali hizo na kufika hatua ya robo fainali.

Katika mechi ya kwanza ha hatua ya makundi, Serengeti Girls ikiwa Kundi D ilikubali kichapo cha mabao 4-0, lakini mechi yake ya pili dhidi ya Ufaransa

INAENDELEA UK . 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002